JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI (PSLE) 2022

# MAARIFA YA JAMII NA STADI ZA KAZI

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI (PSLE) 2022

# 03 MAARIFA YA JAMII NA STADI ZA KAZI

*Kimechapwa na:*
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P. 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

**© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2023**

Haki zote zimehifadhiwa.

YALIYOMO

DIBAJI ..... iv
1.0 UTANGULIZI ..... 1
2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA KILA SWALI 2
2.1 Sehemu A: Maswali ya Kuchagua Jibu Sahihi ..... 2
2.2 Sehemu B: Maswali ya Majibu Mafupi ..... 45
3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA KILA UMAHIRI ..... 56
4.0 HITIMISHO ..... 57
5.0 MAPENDEKEZO ..... 57
Kiambatisho ..... 59

## DIBAJI

Baraza la Mitihani la Tanzania limeandaa taarifa ya uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika Mtihani wa kumaliza Elimu ya Msingi (PSLE) mwaka 2022. Taarifa hii imechambua majibu ya watahiniwa katika somo la Maarifa ya Jamii na Stadi za Kazi. Lengo la taarifa hii ni kutoa mrejesho kwa wanafunzi, walimu, watunga sera, watunga mitaala na wadau wengine wa elimu. Matokeo ya uchambuzi huu ni kiashiria kimojawapo kinachoonesha umahiri ambao watahiniwa waliupata katika elimu yao ya msingi.

Katika taarifa hii, uchambuzi wa kila swali umefanyika na changamoto mbalimbali zilizowapata watahiniwa wakati wa kujibu maswali zimeainishwa. Pia, uchambuzi wa kiwango cha ufaulu kwa kila umahiri umeainishwa ili kuweza kubaini umahiri uliokuwa na changamoto miongoni mwa watahiniwa.

Aidha, uchambuzi umeonesha kuwa watahiniwa waliopata alama za juu walibaini matakwa ya maswali. Wakati watahiniwa waliopata alama za chini walionesha kutokuwa na uwezo wa kubaini matakwa ya maswali. Kwa ujumla, watahiniwa waliofanya vibaya walijibu maswali isivyo sahihi na wengine hawakujibu baadhi ya maswali au walitoa jibu zaidi ya moja kwa swali la 1 – 40, kinyume na maelekezo ya mtihani.

Baraza la Mitihani la Tanzania lina imani kuwa mrejesho huu utawawezesha wadau mbalimbali wa elimu kuchukua hatua madhubuti ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji. Ni matumaini ya Baraza la Mitihani la Tanzania kuwa mamlaka husika zitahakikisha kuwa changamoto zilizoainishwa katika taarifa hii zitapatiwa ufumbuzi ili kuongeza ufaulu kwa watahiniwa kwa siku zijazo.

Baraza la Mitihani la Tanzania linapenda kutoa shukrani za dhati kwa wadau wote waliohusika katika kuandaa taarifa hii.

Dkt. Said A. Mohamed

**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Mtihani wa kumaliza Elimu ya Msingi (PSLE) 2022 wa somo la Maarifa ya Jamii na Stadi za Kazi ulifanyika tarehe 6 Oktoba, 2022. Jumla ya watahiniwa 1,384,186 walisajiliwa kufanya mtihani. Kati yao, watahiniwa 1,350,774 (97.59%) walifanya mtihani, miongoni mwao, watahiniwa 960,178 (71.08%) walifaulu.

Somo la Maarifa ya Jamii na Stadi za Kazi lilikuwa na jumla ya maswali 45 yaliyogawanyika katika sehemu mbili; A na B. sehemu A ilikuwa na maswali 40 ya kuchagua na sehemu B ilikuwa na maswali 5 ya majibu mafupi.

Watahiniwa walitakiwa kujibu maswali yote kutoka katika sehemu zote mbili. Aidha, katika swali la 1 hadi 40 watahiniwa walipewa machaguo matano katika kila swali ambapo kati yake moja lilikuwa jibu sahihi. Watahiniwa walielekezwa kuchagua jibu sahihi na kisha kuweka kivuli kwenye herufi hiyo katika fomu maalum ya kujibia (Optical Mark Reader – OMR). Katika kujibu swali la 41 hadi 45, watahiniwa walielekezwa kuandika majibu yao katika nafasi zilizoachwa wazi kwa kutumia kalamu ya wino wa bluu au mweusi, upande wa nyuma wa karatasi maalum ya OMR.

Katika taarifa hii, herufi ya jibu sahihi kwenye sehemu A imewekwa alama ya nyota (*) katika majedwali na chati. Zaidi ya hayo, idadi na asilimia ya watahiniwa ambao hawakujibu kabisa swali husika, au walichagua jibu zaidi ya moja zimejumuishwa katika uchambuzi na kupewa jina “mengineyo”. Katika uchambuzi huu, idadi ya watahiniwa na asilimia zao katika kila chaguo imeoneshwa. Pia, sababu za usahihi wa jibu na upotofu wa vipotoshi zimeainishwa.

Kigezo cha ukokotoaji wa kiwango cha ufaulu kinategemea idadi ya watahiniwa waliochagua au kuandika jibu sahihi. Ikiwa asilimia 0 hadi 39 ya watahiniwa walichagua au waliandika jibu sahihi, ufaulu katika swali hilo umeelezwa kuwa ni hafifu. Endapo kati ya asilimia 40 hadi 59 ya watahiniwa walichagua au waliandika jibu sahihi, ufaulu katika swali hilo umeelezwa kuwa ni wa wastani. Aidha,

ufaulu katika swali umeelezwa kuwa ni mzuri endapo asilimia 60 au zaidi ya watahiniwa walichagua au waliandika jibu sahihi.

Umahiri uliotahiniwa katika PSLE 2022 katika mtihani wa Maarifa ya Jamii na Stadi za Kazi ni; *Kufuata kanuni za kiuchumi katika shughuli za uzalishaji mali,* swali la 1 - 8 na 41; *Kutumia ramani na elimu ya anga katika maisha ya kila siku,* swali la 9 -13 na 42*; Kutambua misingi ya uzalendo katika jamii,* swali la 14 - 25 na 45*; Kutambua matukio yanayotokea katika mazingira,* swali la 26 - 35 na 43 – 44*; Kutumia misingi ya unadhifu,* swali la 36 na 37*; Kumudu mapishi mbalimbali,* swali la 38*; Kusanifu kazi za sanaa,* swali la 39 na *Kutumia stadi za ujasiriamali,* swali la 40.

## 2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA KILA SWALI

### 2.1 Sehemu A: Maswali ya Kuchagua Jibu Sahihi

**Swali la 1 :** Ubunifu ni kipengele muhimu katika ujasiriamali. Je, nini kitatokea endapo ubunifu utakosekana ?

A Wajasiriamali kukosa motisha
B Polisi kuingilia kati biashara
C Wajasiriamali kupoteza wateja
D Wajasiriamali kuongeza wateja
E Serikali kutunga sheria

**Jedwali Na. 1: Idadi na asilimia ya ufaulu wa watahiniwa kwa kila chaguo**

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 330,521 | 70,820 | 813,101 | 56,648 | 62,954 | 16,730 |
| **Asilimia ya Watahiniwa** | 24.47 | 5.24 | 60.20 | 4.19 | 4.66 | 1.24 |

Swali lilimtaka mtahiniwa kubaini athari itokanayo na kukosekana kwa ubunifu katika biashara. Kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali Na. 1, ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa mzuri kwani

watahiniwa 813,101 (60.28%) walichagua jibu sahihi *C, Wajasiriamari kupoteza wateja*. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa mzuri juu ya kanuni za kiuchumi katika shughuli za kila siku za uzalishaji mali. Walijua kuwa ili kuwavutia wateja ni lazima mjasiriamali awe mbunifu katika biashara ili aweze kushindana na wafanyabiashara wengine.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 70,820 (5.24%) waliochagua kipotoshi *B, Polisi kuingilia kati biashara*; hawakuwa na uelewa mzuri wa stadi za ujasiriamali katika shughuli za kila siku. Kwani polisi kazi zake mahususi ni kuhakikisha usalama wa raia na mali zao. Uchaguzi wa kipotoshi hiki ulionesha kuwa watahiniwa walikosa umahiri kuhusu kazi ya ubunifu katika biashara. Pia hawakuweza kubainisha kazi za polisi katika jamii.


Vivyo hivyo, watahiniwa 330,521 (24.47%) waliochagua kipotoshi *A, Wajasiriamali kukosa motisha*, hawakuwa na uelewa mpana juu ya dhana ya motisha. Kwani, motisha inahusiana na kunyanyua ari ya kufanya kazi kwa wafanyakazi. Ingawa ubunifu unaweza kuathiri motisha, athari muhimu zaidi ya ukosefu wa ubunifu kwa mfanyabiashara ni kukosa wateja. Wateja ndiyo wanaomfanya aendelee kufanya biashara.

Watahiniwa wengine 56,648 (4.19%) waliochagua kipotoshi *D, Wajasiriamali kuongeza wateja*, hawakuelewa kuwa ubunifu huchangia kwa kiasi kikubwa katika kuwavutia wateja. Pia, watahiniwa 62,954 (4.66%) waliochagua kipotoshi *E, Serikali kutunga sheria,* hawakuwa na uelewa kuwa jukumu la utungaji wa sheria kwa lengo la kukuza na kusimamia ufanyikaji wa biashara ni la serikali. Hivyo, hakuhusiani na ubunifu, jambo ambalo anapaswa kuwa nalo mjasiriamali mwenyewe.

Swali la 2 : Je, mjasiriamali ni mtu wa namna gani ?

A Mwenye kukata tamaa upesi
B Mwenye kutegemea mawazo ya wengine
C Mwenye matumaini ya kuwa tajiri kwa haraka
D Mwenye kukasirika haraka apatapo hasara
E Mwenye kutumia fursa vizuri

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kubaini moja ya sifa ya mjasiriamali. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa mzuri kwani watahiniwa 997,799 (73.87%) walichagua jibu sahihi *E, Mwenye kutumia fursa vizuri*. Watahiniwa hao walielewa vizuri dhana ya ujasiriamali. Walielewa kuwa, mjasiriamali hutumia fursa zilizopo kwa ufanisi. Ufafanuzi wa ufaulu wa watahiniwa katika swali hilo umeoneshwa katika Chati Na. 1.




**Chati Na. 1:** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 2*

Kwa upande mwingine, watahiniwa 46,738 (3.46%) walichagua kipotoshi *A, Mwenye kukata tamaa upesi.* Watahiniwa hao hawakuwa na uelewa wa dhana ya mjasiriamali. Kwani kukata tamaa ni kinyume cha sifa za mjasiriamali. Mjasiriamali ni mtu asiyekata tamaa upesi, mbunifu, mvumilivu na mwenye uthubutu wa kujaribu mara nyingi anapopata changamoto hadi lengo litimie.

Pia, watahiniwa 88,661 (6.56%) waliochagua kipotoshi *B, Mwenye kutegemea mawazo ya wengine*, hawakuwa na umahiri wa kutosha kuhusu sifa za mjasiriamali. Kwani, mjasiriamali hapaswi kutegemea mawazo ya mtu mwingine. Vivyo hivyo, watahiniwa 163,494 (12.10%) waliochagua kipotoshi *C, Mwenye matumaini ya kuwa tajiri*


*haraka*, hawakuzingatia sifa ya mjasiriamali ya kuwa na subira na uvumilivu.

Watahiniwa 41,928 (3.10%) waliochagua kipotoshi *D, mwenye kukasirika haraka apatapo hasara,* walikuwa na uelewa mdogo wa sifa za mjasiriamali. Hasira za haraka zina matokeo hasi kwa mjasiriamali. Mjasiriamali anapaswa kuwa mvumilivu, kutafakari makosa, kurekebisha na kisha kuendelea na biashara.

Swali la 3: Amani ni mjasiriamali ambaye ameajiri watu wanne kwenye biashara zake. Je, huo ni aina gani ya ujasiriamali?

| | | |
|---|---|---|
| A Kati | B Mdogomdogo | C Mdogo |
| D Mkubwa | E Makini | |

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kubaini aina gani ya mjasiriamali anayeajiri wafanyakazi wanne. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa hafifu kwani, watahiniwa 1,006,624 (74.52%) walichagua vipotoshi *A Kati, C, Mdogo na D, Mkubwa*. Watahiniwa hao hawakuwa mahiri kuhusu idadi ya wafanyakazi na kiasi cha mtaji kinachobainisha kila kundi la ujasiriamali. Hii ni kutokana na ukweli kwamba, kundi la kati la ujasiriamali biashara huajiri wafanyakazi kati ya 50 mpaka 99. Kundi la wajasiriamali biashara wakubwa huajiri wafanyakazi kuanzia mia moja na kuendelea na kundi la ujasiriamali biashara mdogo lina uwezo wa kuajiri wafanyakazi 5 hadi 49. Aidha, watahiniwa 66,294 (4.91%) waliochagua kipotoshi *E, Makini,* hawakuwa na uelewa juu ya makundi ya wajasiriamali biashara. Kwani, jibu hili halikuwa na uhusiano kabisa na aina ya makundi ya wajasiliamali biashara bali, linahusiana na sifa za mjasiriamali kuwa makini katika kufanya kazi. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili umeoneshwa katika Chati Na. 2.




**Chati Na. 2**: *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 3*

Pamoja na ufaulu hafifu, watahiniwa 259,359 (19.20%) waliochagua jibu sahihi *B, Mdogomdogo* walikuwa na uelewa mzuri juu ya makundi ya ujasiriamali. Watahiniwa hao waliweza kutofautisha kati ya kundi moja na jingine. Hivyo, walibainisha kuwa aina hiyo ya ujasiliamali huajiri wafanyakazi kati ya 1 hadi 4.

**Swali la 4**: Ardhi ni rasilimali ambayo isipotunzwa vizuri inaweza kusababisha hatari katika maisha ya viumbe hai na rasilimali nyingine. Ipi ni njia bora itakayotumika kutunza rasilimali hiyo?

A Kuongeza idadi ya wakulima mashambani
B Kutoa elimu juu ya uhifadhi na utunzaji wa ardhi
C Wananchi kuhimizwa kutumia mbolea za viwandani
D Kuacha kupanda miti katika maeneo ya wazi
E Kuhimiza wafugaji kuongeza idadi ya mifugo

Swali hilo lilimtaka mtahiniwa kubaini njia bora ya kutunza ardhi ili kulinda maisha ya viumbe hai na rasilimali nyingine. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa mzuri, kwani watahiniwa 1,102,437(81.62%), walichagua jibu sahihi *B, Kutoa elimu juu ya uhifadhi na utunzaji wa ardhi*. Watahiniwa hao walifahamu kuwa elimu ni jambo la msingi katika kupata maarifa na ujuzi, hivyo kuitumia katika uhifadhi wa mazingira na ardhi kwa ujumla.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 71,181 (5.27%) walichagua kipotoshi *A, Kuongeza idadi ya wakulima mashambani*. Watahiniwa hao hawakuwa mahiri juu ya dhana nzima ya njia za kutunza rasilimali ardhi. Kuongeza idadi ya wakulima siyo moja ya njia za kutunza rasilimali ardhi, bali ni kuiharibu ikiwa kanuni za kilimo bora hazitazingatiwa.

Vilevile, watahiniwa 69,439 (5.14%) waliochagua kipotoshi *C, Wananchi kuhimizwa kutumia mbolea za viwandani*, walikosa umahiri wa kutosha kuhusu uhifadhi wa rasilimali ardhi. Matumizi ya mbolea za viwandani yasiyofuata mwongozo kutoka kwa Maafisa Ugani huharibu rutuba ya ardhi.

Vivyo hivyo, watahiniwa 52,724 (3.90%) waliochagua kipotoshi *D, Kuacha kupanda miti katika maeneo ya wazi* na watahiniwa 41,780 (3.09%) waliochagua kipotoshi *E, Kuhimiza wafugaji kuongeza idadi ya mifugo* walikosa umahiri juu ya namna bora za utunzaji wa rasilimali ardhi. Ardhi inapokosa uoto wa aina yoyote huathiriwa kwa urahisi na maji au upepo na kusababisha mmomonyoko wa udongo na hatimaye uharibifu wa mazingira. Idadi kubwa ya mifugo husababisha uharibifu wa mazingira na ardhi kwani hutifua udongo ambao huathiriwa kirahisi na mmomonyoko wa udongo.

**Swali la 5**: Tanzania imebahatika kuwa na rasilimali nyingi, mojawapo imebeba nyinginezo katika mazingira. Rasilimali hiyo ni ipi?

A Madini B Misitu C Mifugo
D Mbuga za wanyama E Ardhi

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kubaini rasilimali ambayo imebeba rasilimali nyingine. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa wa wastani kwani watahiniwa 706,871 (52.33%) walichagua jibu sahihi *E, Ardhi*. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu rasilimali zinazopatikana Tanzania. Walielewa kuwa ardhi imebeba rasilimali za asili na zisizo za asili. Ardhi ndio rasilimali ambayo madini, misitu, mifugo, mbuga za wanyama na hifadhi za wanyama na viumbe mbalimbali hupatikana. Lakini pia, shughuli mbalimbali za

binadamu kama vile kilimo, ufugaji, uchimbaji wa madini na upasuaji wa mbao hufanyika katika ardhi.

Hata hivyo, watahiniwa 624,375 (46.22%) walichagua kipotoshi *A, Madini, B, Misitu, C, Mifugo, D, Mbuga za Wanyama*. Watahiniwa hao hawakuelewa kuwa rasilimali zote hizi zimebebwa na ardhi na kwamba haiwezekani kueleza kuhusu madini, misitu, mifugo na wanyamapori bila kugusa ardhi. Kwani ardhi ina uhusiano wa moja kwa moja na rasilimali zote hizo.

**Swali la 6**: Mwalimu Kasese aliwaambia wanafunzi wake wataje madini na mikoa yanapopatikana nchini Tanzania. Je, walitaja mkoa gani ambapo makaa ya mawe yanapatikana?

A Manyara B Mbeya C Kagera
D Morogoro E Mara


Swali hili lilimtaka mtahiniwa kubaini mkoa ambao makaa ya mawe yanapatikana nchini Tanzania. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa hafifu kwani watahiniwa 995,319 (73.69%) walichagua vipotoshi *A, Manyara, C, Kagera, D, Morogoro na E, Mara*. Watahiniwa hao hawakuelewa kuwa, makaa ya mawe hayapatikani katika mikoa hiyo. Aidha, hawakubaini aina ya rasilimali inayopatikana katika mikoa hiyo ambapo, katika mkoa wa Manyara kuna Tanzanite, Kagera kuna Bati, Morogoro kuna Rubi na Mara kuna Dhahabu. Hii iliwafanya washindwe kutambua mkoa ambao makaa ya mawe yanapatikana.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 332,144 (24.59%) walichagua jibu sahihi B, Mbeya. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa kuhusu aina mbalimbali za madini na mikoa ambayo yanapatikana nchini Tanzania. Hii iliwawezesha kutambua kuwa makaa ya mawe yanapatikana mkoani Mbeya.

**Swali la 7**: Wakati wa kipindi, mwalimu aliwataka wanafunzi wataje fursa za kibiashara zinazoweza kupatikana pembezoni mwa bahari ya Hindi. Lipi kati ya yafuatayo lingekuwa jibu lao?

A Kutengeneza mikanda ya ngozi
B Kuzalisha maziwa
C Kuuza dawa ya mifugo
D Kuuza ngozi za wanyama
E Utalii

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kubaini fursa za kibiashara zinazoweza kupatikana pembezoni mwa bahari ya Hindi. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa wa wastani kwani, watahiniwa 792,841 (58.70%) walichagua jibu sahihi *E, Utalii*. Watahiniwa hao walikuwa na ufahamu mzuri kuhusu vivutio vya utalii zikiwemo fukwe za bahari. Fukwe hizo zimekuwa maarufu na vivutio vikubwa vya watalii wa ndani na nje ya nchi. Watalii huvutiwa na fukwe hizi kutokana na uwepo wa maeneo ya kuogelea, nyumba za sanaa na hoteli za kifahari. Hivyo, wafanyabiashara hunufaika kwa kupata pesa. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili umeoneshwa katika Chati Na. 3.




**Chati Na. 3**: *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 7*

Kwa upande mwingine, jumla ya watahiniwa 537,627 (39.80%) walichagua vipotoshi *A, Kutengeneza mikanda ya Ngozi; B, Kuzalisha maziwa; C, Kuuza dawa za mifugo na D, Kuuza Ngozi za*

*Wanyama.* Watahiniwa hao hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu fursa mbalimbali zinazopatikana maeneo tofauti kwasababu vipotoshi hivyo vinahusiana na mazao yatokanayo na mifugo na dawa za mifugo. Hata hivyo, maeneo yanayohusika na uzalishaji wake yapo mbali na bahari.

**Swali la 8**: Mwalimu Timamu alifundisha kuhusu kilimo cha mazao ya biashara kilichofanywa Tanganyika kabla ya uhuru. Je wanafunzi walifundishwa mazao yapi?

A Zabibu, kahawa, chai na maharage
B Mahindi, kahawa, chai na pareto
C Kahawa, pareto, mkonge na chai
D Pareto, korosho, chai na mahindi
E Korosho, maharage, mkonge na pareto

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kubaini mazao ya biashara yaliyokuwa yakilimwa Tanganyika kabla ya uhuru. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hilo ulikuwa wa wastani kwani, jumla ya watahiniwa 774,575 (57.34%) walichagua jibu sahihi *C, Kahawa, pareto, mkonge na chai*. Watahiniwa hao walikuwa na ufahamu mzuri kutokana na kuwa na umahiri kuhusu shughuli za uzalishaji wa mazao ya biashara Tanganyika kabla ya uhuru. Wakoloni walijishughulisha na kilimo cha mazao ya biashara kwani yalikuwa malighafi muhimu ya viwanda katika mataifa ya Ulaya. Pia, watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutofautisha mazao ya biashara na ya chakula.

Watahiniwa wengine, 558,058 (41.31%) waliochagua vipotoshi *A, Zabibu, kahawa, chai na maharage; B, Mahindi, kahawa, chai na pareto; D, Pareto, korosho, chai na mahindi*, na *E, Korosho, maharage, mkonge na pareto* walikosa umahiri wa kubaini mazao ya chakula yaliyokuwa katika vipotoshi hivyo. Kwani vipotoshi hivyo vyote vilihusisha maharage na mahindi ambayo ni mazao ya chakula.

**Swali la 9**: Inapendekezwa kuwa shughuli za kibinadamu ziwe rafiki kwa mazingira ili kuzuia kuharibika kwa tabaka la ozoni. Ni shughuli ipi sahihi katika kulinda tabaka hilo?

A Kufuga mifugo mingi katika eneo dogo
B Kuvua kwa kutumia baruti
C Uchimbaji wa madini
D Upandaji wa miti
E Kutumia mbolea za viwandani kwa wingi

Katika swali hili, mtahiniwa alitakiwa kubaini shughuli sahihi katika kulinda tabaka la ozoni. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa mzuri kwani watahiniwa 1,047,066 (77.52%) walichagua jibu sahihi *D, Upandaji wa miti*. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa mzuri juu ya dhana ya utunzaji wa mazingira na hasa utunzaji wa angahewa. Pia, walifahamu kwamba miti husaidia kunyonya kabonidioksaidi na kabonimonoksaidi ambazo huharibu tabaka la ozoni.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 73,286 (5.43%) waliochagua kipotoshi *A, Kufuga mifugo mingi katika eneo dogo*, hawakuwa na uelewa kuhusu utunzaji wa mazingira ya anga. Kwani, kufuga mifugo mingi katika eneo dogo husababisha uharibifu wa tabaka la juu la ardhi na mimea. Hii husababisha mmomonyoko wa udongo na uharibifu wa mazingira ambao unasababisha uharibifu wa tabaka la ozoni.

Vivyo hivyo, watahiniwa 61,493 (4.55%) waliochagua kipotoshi *B, Kuvua kwa kutumia baruti*, hawakuelewa athari za uvuvi wa aina hiyo. Matumizi ya baruti huharibu mfumo wa ikolojia, kwani huua hata viumbe wasiokusudiwa kuuwawa na huharibu mazalia yao. Watahiniwa wengine 153,624 (11.37%) waliochagua vipotoshi *C, Uchimbaji wa madini* na *E, Kutumia mbolea za viwandani*, hawakuzingatia athari za shughuli hizo. Uchimbaji wa madini husababisha uharibifu wa ardhi na mbolea za viwandani zinaharibu uwiano mzuri wa kemikali kwenye ardhi na kuifanya ardhi kutokuwa na rutuba.

**Swali la 10**: Mwalimu alifundisha umuhimu wa tabaka la ozoni kwa maisha ya viumbe hai na vitu vinavyoathiri uimara wa tabaka la ozoni. Je mwalimu alitaja kitu gani kinachoathiri uimara wa tabaka la ozoni?

A Upepo B Hewa ya oksijeni C Radi
D Mvua E Gesi ya kloroflorokaboni

**Jedwali Na. 2: Idadi na asilimia ya ufaulu wa watahiniwa kwa kila chaguo**

| Chaguo | A | B | C | D | E* | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 108,114 | 125,694 | 208,241 | 85,810 | 803,733 | 19,182 |
| **Asilimia ya Watahiniwa** | 8.00 | 9.31 | 15.42 | 6.35 | 59.50 | 1.42 |

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kubainisha kitu kinachoathiri uimara wa tabaka la ozoni. Kama Jedwali Na. 2 linavyoonesha, ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa wa wastani kwani watahiniwa 803,733 (59.50%) walichagua jibu sahihi *E, Gesi ya kloroflorokaboni*. Watahiniwa hao walikuwa na ufahamu mzuri juu ya angahewa na athari zitokanazo na shughuli za viwandani kwenye mazingira. Aidha, walielewa kuwa viwanda huzalisha gesi za kloroflorokaboni, kabonidayoksaidi na kabonimonoksaidi, ambazo zikifika kwenye angahewa la kati huharibu tabaka la ozoni.

Kwa upande mwingine, jumla ya watahiniwa 527,859 (39.08%) walichagua vipotoshi *A, Upepo; B, Hewa ya oksijeni; C, Radi na D, Mvua*. Watahiniwa hawa walikosa umahiri wa dhana ya utunzaji wa mazingira na athari zitokanazo na shughuli za viwanda. Kwani upepo, hewa ya oksijeni, radi na mvua siyo zao la shughuli za viwandani, hupatikana kwa asili na haviathiri tabaka la ozoni.

**Swali la 11**: Meli ya mizigo iliyoko mji wa Brasilia $45^0$ Magharibi huanza safari siku ya Jumatatu saa 4:00 usiku. Muda huo utakuwa ni saa ngapi katika mji wa Kabul ulioko $75^0$ Mashariki?

A Jumatatu 6:00 usiku
B Jumanne 5:00 usiku
C Jumanne 12:00 asubuhi
D Jumatatu 6:00 mchana
E Jumanne 12:00 jioni

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kukokotoa utofauti wa muda kati ya miji miwili ili kubaini muda wa mji ambao haukubainishwa. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa hafifu kwani watahiniwa 833,066 (61.67%) walichagua vipotoshi *E, Jumanne 12:00 jioni; A, Jumatatu 6:00 usiku; B, Jumanne 5:00 usiku na D, Jumatatu 6:00 mchana*. Watahiniwa hao walikosa umahiri wa ukokotoaji wa masaa.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 490,873 (36.34%) walichagua jibu sahihi *C, Jumanne 12:00 asubuhi*. Watahiniwa hao walikokotoa tofauti ya muda kati ya miji hiyo miwili na kubainisha muda katika jiji la Kabul. Waliweza kujumlisha nyuzi za mji wa Brasilia na Kabul ($45^0 + 75^0 = 120^0$). Walihusisha nyuzi na dakika ambapo, nyuzi $15^0$ = ni sawa na dakika 60. Hivyo, nyuzi $120^0$ ni sawa na saa 8. Saa zilizopatikana zilijumlishwa na 8 na hivyo kupata jibu sahihi ambalo ni saa 12.00 asubuhi. Hivyo, kwa kuwa Kabul iko Mashariki ya Greenwich itakuwa Jumanne saa 12:00 asubuhi.

**Swali la 12** : Mwalimu Kulwa aliwafundisha wanafunzi wake kuhusu mistari ya kufikirika inayochorwa katika ramani. Je, ni mistari ipi aliwafundisha kuwa huchorwa kutoka upande wa Kaskazini kuelekea Kusini?

A Tropiki
B Latitudo
C Mstarihi
D Longitudo
E Ikweta

**Jedwali Na. 3: Idadi na asilimia ya ufaulu wa watahiniwa kwa kila chaguo**

| Chaguo | A | B | C | D* | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 110,252 | 300,410 | 104,541 | 466,222 | 344,167 | 25.182 |
| **Asilimia ya Watahiniwa** | 8.16 | 22.24 | 7.74 | 34.52 | 25.48 | 1.86 |

Swali lilimtaka mtahiniwa kubaini mistari ya kufikilika ambayo huchorwa kutoka upande wa Kaskazini kuelekea Kusini katika ramani. Kama jedwali Na. 3 linavyoonesha, ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa hafifu kwani watahiniwa 859,370 (63.62%) hawakuchagua jibu sahihi. Kati yao, watahiniwa 300,410 (22.24%) walichagua vipotoshi *B, Latitudo* na *E, Ikweta*. Watahiniwa hao walishindwa kutofautisha mistari ya kufikirika inayochorwa kutoka Kaskazini kuelekea Kusini na mistari inayochorwa kutoka Magharibi kuelekea Mashariki (longitudo na latitudo). Kwani, mistari ya latitudo ikiwepo wa Ikweta huchorwa kutoka Magharibi kwenda Mashariki. Aidha, watahiniwa 110,252 (8.16%.) waliochagua kipotoshi *A, Tropiki* hawakuwa na uelewa kuwa, Tropiki ni ukanda wa Kaskazini au Kusini mwa Ikweta. Vile vile, watahiniwa 104,541 (7.74%) waliochagua kipotoshi *C, Mstarihi* hawakuwa na uelewa juu ya mstari huu kwani Mstarihi ni mstari wa tarehe wa kimataifa ambao kupitia mstari huo, tarehe na siku hubadilika. Unapouvuka msitarihi kuelekea upande wa Mashariki siku hupungua na unapouvuka kuelekea upande wa Magharibi siku huongezeka.

Pamoja na watahiniwa wengi kukosa swali hili, watahiniwa 466,222 (34.52%) walichagua jibu sahihi *D*, Longitudo. Watahiniwa hao walifahamu sifa za mistari ya Latitudo na Longitudo inayochorwa katika ramani, hivyo kuweza kubaini jibu sahihi.

**Swali la 13**: Jasiri anayeishi katika mji wa Handani, alianza kuangalia mechi katika televisheni saa 9:00 alasiri na rafiki yake Juhudi anayeishi katika mji wa Mikoko uliopo $40^0$ Mashariki, alianza kuangalia mechi hiyo saa 7:00 mchana. Je, mji wa Handani upo Longitudo ngapi?

A $70^0$ Magharibi
B $30^0$ Magharibi
C $90^0$ Mashariki
D $70^0$ Mashariki
E $30^0$ Mashariki


Swali hili lilimtaka mtahiniwa kubaini nyuzi za mji wa Handani. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa hafifu kwani jumla ya watahiniwa 1,063,680 (63.22%) walichagua vipotoshi *A, $70^0$ Magharibi; B, $30^0$ Magharibi; C $90^0$ Mashariki* na *E, $30^0$* Mashariki. Watahiniwa hao walishindwa kukokotoa tofauti ya masaa kati ya miji ya Handani na Mikoko ili hatimaye watumie tofauti hiyo kupata nyuzi za Longitudo. Aidha, walishindwa kujumlisha nyuzi za mji wa Mikoko ($40^0$) ambazo zinachukua masaa mawili ($30^0$) ili kupata za mji wa Handani.

Hata hivyo, watahiniwa 258,987 (19.17%) walichagua jibu sahihi *D, $70^0$ Mashariki*. Watahiniwa hao walitafuta tofauti ya nyuzi baina ya miji hiyo miwili. Hivyo, walikokotoa tofauti ya saa kati ya miji hiyo miwili (9 - 7= saa 2) na kisha kubadilisha tofauti hiyo katika nyuzi. Walikokotoa na kupata nyuzi 30 kwa kuwa, saa moja ni sawa na nyuzi 15. Hivyo walizidisha nyuzi 15 kwa saa mbili na kupata nyuzi 30. Hatimaye walijumlisha nyuzi za miji miwili $40^0 + 30^0 = 70^0$ na kubaini kuwa, mji wa Handani upo nyuzi $70^0$.

**Swali la 14**: Bara la Afrika lina mashujaa wengi ambao walipinga ukoloni mamboleo. Mashujaa gani wa Afrika Mashariki waliopinga ukoloni huo?

A Jomo Kenyatta, Patrice Lumumba na Samora Machel
B Julius K. Nyerere, Kwame Nkrumah na Nelson Mandela
C Jomo Kenyatta, Julius. K. Nyerere na Milton Obote
D Patrice Lumumba, Julius. K. Nyerere na Kwame Nkrumah
E Jomo Kenyatta, Kamuzu Banda na Samora Machel

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kuwatambua mashujaa wa Afrika Mashariki waliopinga ukoloni mamboleo. Ufaulu katika swali hili ulikuwa hafifu kwani watahiniwa 377,456 (27.94%) pekee ndiyo waliochagua jibu sahihi *C, Jomo Kenyatta, Julius K. Nyerere na Milton Obote*. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili umeoneshwa katika Chati Na. 4.




**Chati Na. 4**: *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 14*

Watahiniwa 949,731 (70.31%) walichagua vipotoshi A, B, D na C. Kati yao, watahiniwa 155,970 (11.55%) waliochagua kipotoshi *A Jomo Kenyatta, Patrice Lumumba na Samora Machel*, walikosa ufahamu wa kanda za Afrika. Katika uchaguzi huu, ni kiongozi

mmoja tu Jomo Kenyatta ndiye aliyetokea Afrika Mashariki. Patrice Lumumba ni shujaa wa Jamhuri ya Kongo ambayo inapatikana Afrika ya Kati na Samora Machel ni shujaa wa Msumbiji ambayo iko Kusini mwa Afrika.

Pia, watahiniwa 688,851 (50.99%) walichagua *vipotoshi B, Julius K. Nyerere, Kwame Nkrumah na Nelson Mandela* na *D, Patrice Lumumba, Julius K. Nyerere na Kwame Nkrumah*. Watahiniwa hao hawakutambua kuwa, Kwame Nkrumah anatokea Ghana (Afrika Magharibi) na Nelson Mandela ni wa Jamhuri ya Afrika ya Kusini ambayo iko Kusini mwa bara la Afrika. Aidha, watahiniwa 104,910 (7.77%) waliochagua kipotoshi *E, Jomo Kenyatta, Kamuzu Banda na Samora Machel*, hawakubaini kuwa Kamuzu Banda ni wa Malawi na Samora Machel ni wa Msumbiji ambapo wote ni wa ukanda Kusini mwa Afrika.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 377,456 (27.94%) walichagua jibu sahihi *C, Jomo Kenyatta, Julius K. Nyerere na Milton Obote*. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa juu ya mashujaa waliopinga ukoloni mamboleo katika Afrika Mashariki. Aidha, waliweza kuwatofautisha mashujaa wa Afrika Mashariki na mashujaa wa maeneo mengine ya Afrika.

**Swali la 15** : Tanzania imeongozwa na mawaziri wakuu wengi tangu uhuru. Je, mawaziri wapi walishika nyazifa wakati wa Mwalimu Nyerere?

A Rashid Mfaume Kawawa na Joseph Sinde Warioba

B Rashid Mfaume Kawawa na Edward Moringe Sokoine

C John Samweli Malecela na Mizengo Kayanza Pinda

D Edward Ngoyai Lowassa na Cleopa David Msuya

E Edward Moringe Sokoine na Fredrick Sumaye

**Jedwali Na. 4: Idadi na asilimia ya ufaulu wa watahiniwa kwa kila chaguo**

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 226,644 | 744,187 | 120,151 | 102,341 | 141,681 | 15,770 |
| **Asilimia ya Watahiniwa** | 16.78 | 55.09 | 8.89 | 7.58 | 10.49 | 1.17 |

Swali lilimtaka mtahiniwa kubaini mawaziri ambao walishika nyadhifa wakati wa utawala wa Raisi Mwalimu Nyerere. Kama Jedwali Na. 4 linavyoonesha, ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa wastani kwani watahiniwa 744,187 (55.09%) walichagua jibu sahihi *B, Rashid Mfaume Kawawa*, na *Edward Moringe Sokoine*. Watahiniwa hao walidhihirisha uelewa wa kutosha juu ya mawaziri walioongoza na kushika madaraka wakati wa Raisi Mwalimu Julius K. Nyerere aliyetawala kuanzia mwaka 1961 hadi 1985.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 226,644 (16.78%) waliochagua kipotoshi *A, Rashid Mfaume Kawawa na Joseph Sinde Warioba* hawakuelewa kuwa, Joseph Sinde Warioba alikuwa Waziri Mkuu kipindi cha utawala wa Raisi Ally Hassan Mwinyi. Watahiniwa 120,151 (8.89%) waliochagua kipotoshi *C, John Samwel Malecela na Mizengo Kayanza Pinda*, hawakuwa sahihi kwa kuwa John Samwel Malecela alikuwa Waziri Mkuu wakati wa utawala wa Rais Mwinyi na Mizengo Kayanza Pinda alikuwa Waziri Mkuu wakati wa utawala wa Rais Jakaya Mrisho Kikwete.

Aidha, watahiniwa 102,341 (7.58%) walichagua vipotoshi *D, Edward Ngoyai Lowassa na Cleopa David Msuya*. Watahiniwa hao walishindwa kubaini kuwa Edward Ngoyai Lowassa alikuwa Waziri Mkuu wakati wa Raisi Jakaya Mrisho Kikwete, na Cleopa David Msuya alikuwa Waziri Mkuu enzi za Rais Ally Hassan Mwinyi. Vivyo hivyo, watahiniwa 141,681 (10.49%) walichagua kipotoshi *E, Edward Moringe Sokoine na Fredrick Sumaye*. Watahiniwa hao hawakuwa na uelewa kuwa, Fredrick Sumaye alikuwa Waziri Mkuu katika utawala wa Rais Benjamin William Mkapa.

**Swali la 16**: Ni kwa jinsi gani Uganda ilipata uhuru wake?

A Kupitia vita vya msituni
B Kupitia mapinduzi
C Kupitia vita
D Kupitia njia ya Katiba
E Kupitia ushirikiano

Swali lilimtaka mtahiniwa kutambua namna ambayo nchi ya Uganda ilipata uhuru. Ufaulu katika swali hili ulikuwa hafifu kwani watahiniwa 1,115,885 (81.87%) walichagua vipotoshi. Kati yao, 79,558 (5.89%) waliochagua kipotoshi *A, Kupitia vita vya msituni*. Watahiniwa hao hawakutofautisha njia ya katiba katika kupigania uhuru na mapambano ya msituni. Uchaguzi wa kipotoshi hiki unaweza kuwa umesababishwa na uwepo wa mapinduzi ya kijeshi yaliyoikumba nchi hiyo mara baada ya uhuru.

Watahiniwa wengine 281,501 (20.84%) waliochagua kipotoshi *B, Kupitia mapinduzi*, walikosa ufahamu wa dhana ya mapinduzi. Kwani mapinduzi ni kitendo cha kuutoa utawala uliopo madarakani kwa nguvu na mara nyingi hufanyika kwa upande mwingine wa kisiasa kitendo hiki hufanyika kwa njia ya vurugu au vita. Zipo nchi chache barani Afrika zilizopata uhuru kwa njia ya mapinduzi ambazo ni Misri mwaka 1952 na Zanzibar mwaka 1964.


Vivyo hivyo, watahiniwa 620,582 (45.94%) waliochagua kipotoshi *C, Kupitia Vita*, walikuwa hawajui kuwa Uganda haikupata uhuru wake kwa njia ya vita. Kwa upande wa watahiniwa 124,244 (9.20%) waliovutiwa na kipotoshi *E, Kupitia Ushirikiano*, walikosa uelewa kuwa ushirikiano ambao wakoloni walifanya urafiki na baadhi ya makabila dhaifu ya Kiafrika ulilenga kuwawezesha kuyateka na kuyatawala makabila yenye nguvu.

Pamoja na watahiniwa wengi (81.87%) kushindwa kuchagua jibu sahihi, watahiniwa 221,586 (17.00%) walichagua jibu sahihi *D, Kupitia njia ya katiba*. Watahiwa hao walikuwa na maarifa yaliyowawezesha kutambua kuwa uhuru wa nchi ya Uganda ulipatikana kwa njia ya katiba chini ya Rais Miltone Obote mwaka 1962.

**Swali la 17**: Kiongozi yupi aliongoza mapambano ya kudai uhuru wa watu weusi nchini Afika ya Kusini?

A Julius Kambarage Nyerere
B De Clerk
C Keneth Kaunda
D Nelson Mandela
E Kwame Nkurumah

Swali lilimtaka mtahiniwa kubaini kiongozi aliyeongoza mapambano ya kudai uhuru wa watu weusi nchini Afrika ya Kusini. Ufaulu katika swali hili ulikuwa wa wastani kwani, watahiniwa 629,220 (46.58%) walichagua jibu sahihi *D, Nelson Mandela*. Watahiniwa hao walielewa kuwa Nelson Mandela ndiye aliyeongoza harakati za ukombozi wa watu weusi dhidi ya ubaguzi wa rangi katika nchi ya Afrika Kusini. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili umeoneshwa katika Chati Na. 5.




**Chati Na. 5**: *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 17*

Jumla ya watahiniwa 361,827 (26.79%) walichagua kipotoshi *A, Julius Kambarage Nyerere*. Watahiniwa hao hawakubaini kuwa Julius K. Nyerere hakuwa kiongozi anayetokea nchi ya Afrika ya Kusini, bali ni mwasisi wa Taifa la Tanzania lililopata uhuru wake mwaka 1961. Vivyo hivyo, watahiniwa 104,148 (7.71%) walichagua kipotoshi *B, De Clerk*. Watahiniwa hawa hawakubaini kuwa De Clerk alikuwa kiongozi wa serikali dhalimu ya makaburu nchini Afrika ya Kusini toka mwaka 1989 hadi mwaka 1994.

Watahiniwa wengine, 130,111 (9.63%) waliochagua kipotoshi *C, Keneth Kaunda*, hawakubaini kuwa Kaunda alikuwa ni Rais wa Zambia. Aidha, watahiniwa 106,154 (7.86%) walichagua kipotoshi *E, Kwame Nkrumah*. Hata hivyo, Nkrumah alikuwa mwasisi wa nchi ya Ghana. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa mdogo juu ya viongozi mbalimbali na nchi walioongoza katika mapambano ya kudai uhuru.

**Swali la 18**: Katika karne ya 19, Pwani ya Afrika Mashariki ilitembelewa na wageni wengi kutoka Bara la Asia. Nini lilikuwa lengo lao kuu?

A Shughuli za kijeshi
B Shughuli za kisiasa
C Shughuli za kiutamaduni
D Shughuli za kiuchumi
E Shughuli za kijamii

Swali lilimtaka mtahiniwa kutambua lengo kuu la wageni waliofika Afrika Mashariki kutokea Bara la Asia katika karne ya 19. Ufaulu ulikuwa mzuri kwani watahiniwa 853,492 (63.19%) walichagua jibu sahihi *D, Shughuli za kiuchumi*. Watahiniwa hao, walikuwa na maarifa juu ya malengo ya wageni kutoka Bara la Asia kuja Pwani ya Afrika Mashariki. Wageni hao walitoka nchi za Siria, Iran, Oman, Yemen, China, Indonesia na India. Wageni hao walifanya biashara za watumwa, nta, mpira, pembe za ndovu na ngozi. Aidha, walileta nguo, shanga, sabuni, vikombe, visu, mapanga, mchele, bunduki na vyombo vya nyumbani katika Pwani ya Afrika Mashariki.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 481,542 (35.65%) waliochagua vipotoshi *A, Shughuli za kijeshi; B, Shughuli za kisiasa; C, Shughuli za kiutamaduni* na *E, Shughuli za kijamii*, walidhihirisha uelewa mdogo wa madhumuni ya kuja kwa wageni kutoka Asia katika Pwani ya Afrika Mashariki. Waasia walikuja Pwani ya Afrika Mashariki kwa lengo la shughuli za kiuchumi, hasa biashara na siyo kwaajili ya shughuli za kijeshi, kisiasa, kitamaduni na kijamii.

**Swali la 19**: Kwa nini Wareno walijenga ngome nyingi maeneo ya Pwani?

A Kuwalinda Waafrika dhidi ya Waarabu
B Kulinda maslahi yao ya kibiashara
C Kuwalinda Waarabu wasivamiwe na Waafrika
D Kuonesha nguvu zao za kijeshi kwa Waafrika
E Kuwafundisha Waafrika mbinu za kijeshi

Swali lilimtaka mtahiniwa kutambua sababu iliyowafanya Wareno kujenga Ngome nyingi maeneo ya Pwani. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa mzuri kwani watahiniwa 838,978 (62.11%) waliweza kuchagua jibu sahihi *B, Kulinda maslahi yao ya kibiashara*. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa sahihi juu ya umuhimu wa Ngome za Wareno zilizojengwa katika maeneo ya Pwani. Ngome hizo zilijengwa ili kuimarisha ulinzi wa maeneo waliyoyadhibiti.

Jumla ya watahiniwa 157,568 (11.67%) walichagua kipotoshi *A, Kuwalinda Waafrika dhidi ya Waaarabu*. Watahiniwa hao walishindwa kutambua kuwa Wareno hawakuwa na lengo la kuwalinda Waafrika, bali walijikita katika kuwanyonya kibiashara kwa kuchukua bidhaa zenye thamani kubwa na kuwaacha Waafrika katika umaskini uliokithiri.

Zaidi, watahiniwa 114,912 (8.51%) waliochagua kipotoshi *C, Kuwalinda Waarabu wasivamiwe na Waafrika*, hawakuelewa kuwa Waarabu na Wareno walikuwa wafanyabiashara. Hivyo, walikuwa na uhasama wa kimaslahi. Pia, watahiniwa 223,007 (16.51%) waliochagua vipotoshi *D, Kuonesha nguvu zao za kijeshi kwa Waafrika* na *E, Kuwafundisha Waafrika mbinu za kijeshi*, walishindwa kutambua kuwa Wareno hakuwa na malengo ya kuonesha wala kuwafundisha nguvu za kijeshi Waafrika. Hii inaashiria kuwa, watahiniwa hawakuwa na maarifa kuhusu uhusiano wa Waafrika na watu kutoka Ulaya na Asia hadi mwaka 1961.

**Swali la 20**: Fatuma ni binti wa kaka yangu, Casmir ni mtoto wa kiume wa dada wa baba yake Fatuma. Je, Fatuma atamwitaje Casmir?

A Binamu
B Mpwa wa kiume
C Mpwa wa kike
D Mjomba
E Kaka


Swali lilimtaka mtahiniwa kutambua uhusiano uliopo kati ya ndugu wawili; Fatuma na Casmir. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa wa wastani, kwani watahiniwa 627,924 (46.49%) walichagua jibu sahihi *A, Binamu*. Watahiniwa hawa walikuwa na ufahamu kuwa binamu ni mtoto wa shangazi au mjomba. Pia, walikuwa na uelewa wa mahusiano katika familia ambao uliwawezesha kutofautisha kati ya binamu na wengine kama vile mpwa wa kike, mjomba na kaka. Jambo hili linaloonesha kuwa, walikuwa na umahiri kuhusu chanzo na mahusiano ya familia.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 232,939 (17.24%) waliochagua kipotoshi *B, Mpwa wa kiume*, walishindwa kutambua kuwa mpwa wa kiume ni mtoto wa kiume wa kaka au dada. Vilevile, watahiniwa 110,200 (8.16%) waliochagua kipotoshi *C, Mpwa wa kike*, walishindwa kubaini kuwa mpwa wa kike pia ni mtoto wa kaka au dada. Zaidi, watahiniwa 222,937 (16.50%) waliochagua kipotoshi *D, Mjomba* hawakutambua kuwa mjomba ni kaka au mdogo wa kiume wa mama. Vilevile, watahiniwa 137,149 (10.15%) waliochagua kipotoshi *E, Kaka*, hawakubaini kuwa kaka ni ndugu wa damu wa kiume wa kuzaliwa. Kwa ujumla, watahiniwa walioshindwa kuchagua jibu sahihi hawakuelewa namna ndugu wanavyohusiana katika familia.

**Swali la 21**: Katika mapambano ya kudai uhuru Afrika, zipo sababu za ndani na sababu za nje. Ipi ni sababu ya nje?

A Tamaa ya kuondoa utawala wa mabavu
B Kukua kwa unyonyaji wa kikoloni
C Kurudi kwa wanajeshi wa Kiafrika waliopigana vita vya pili vya dunia
D Kukua kwa unyanyasaji unaofanywa na wakoloni
E Kupinga kutawaliwa na huduma hafifu za kijamii

Swali lilimtaka mtahiniwa kubainisha sababu ya nje iliyohamasisha mapambano ya kudai uhuru katika Afrika. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa hafifu kwani jumla ya watahiniwa 1,024,260 (75.82%) walichagua vipotoshi *A, Tamaa ya kuondoa utawala wa mabavu; B, Kukua kwa unyonyaji wa kikoloni; D, Kukua kwa unyanyasaji unaofanywa na wakoloni* na *E, Kupinga kutawaliwa na huduma hafifu za kijamii.* Watahiniwa hao hawakuelewa kuwa vipotoshi hivyo vyote vilihusu sababu za ndani zilizochochea kupigania uhuru wa Afrika. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili umeoneshwa katika Chati Na. 6.




**Chati Na. 6**: *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 21*

Uchambuzi zaidi ulionesha kuwa watahiniwa 306,950 (22.72%) tu walichagua jibu sahihi *C, Kurudi kwa wanajeshi wa Kiafrika waliopigana Vita vya Pili vya Dunia*. Watahiniwa hao walitambua kuwa, wanajeshi waliorudi kutoka Vita vya Pili vya Dunia mwaka 1939 hadi 1945 walihusika kwa kiasi kikubwa katika mapambano ya kudai uhuru. Uzoefu walioupata wakati wa vita ya pili ya dunia uliwawezesha kutambua kuwa wazungu pia hushindwa katika mambo mbalimbali hata kuuawa katika uwanja wa medani.

**Swali la 22**: Mila na desturi za jamii za kale zilikuwa na umuhimu mkubwa katika maisha ya wanajamii. Je, upi ni umuhimu mmojawapo?

A Zilikuza tabia mbaya na kutoheshimiana
B Ziliwaelimisha Waafrika kuwa wakatili na majasiri
C Zilichochea ukatili na ukosefu wa adabu kwa Waafrika
D Zilifundisha kujitegemea, umoja na mshikamano
E Zilisisitiza uharibifu wa mazingira na kujaliana

Swali lilimtaka mtahiniwa kubaini umuhimu wa mila na desturi za kale katika maisha ya wanajamii. Ufaulu wa watahiniwa ulikuwa mzuri kwani watahiniwa 922,580 (68.30%) walichagua jibu sahihi *D, Zilifundisha kujitegemea, umoja na mshikamano*. Watahiniwa hao walitambua tunu za mila na desturi za kale za Kiafrika. Tunu hizi zimekuwa zikitumika katika maisha yao ya kila siku, ambapo wanajamii hushirikiana katika mambo mbalimbali kama vile ngoma, sherehe za harusi na misiba. Hivyo, waliweza kutumia maarifa hayo kujibu swali hili kwa usahihi.

Kwa upande mwingine, jumla ya watahiniwa 413,386 (30.60%) walichagua vipotoshi *A, Zilikuza tabia mbaya na kutoheshimiana; B, Ziliwaelimisha Waafrika kuwa wakatili na majasiri; C, Zilichochea ukatili na ukosefu wa adabu kwa Waafrika* na *E, Zilisisitiza uharibifu wa mazingira na kujaliana*. Watahiniwa hao hawakuwa na umahiri kuhusu umuhimu wa mila na desturi za Kiafrika. Vipotoshi hivi vinahusisha mambo yasiyokubalika katika jamii ambayo ni kutoheshimiana, kuwa wakatili na kukosa adabu, hivyo hayawezi kuwa sehemu ya mila na desturi za jamii za kale. Kipotoshi E, kinauhusisha uharibifu wa mazingira, jambo ambalo halikufanywa na jamii za kale. Mila na desturi zilifundisha namna bora ya kufanya kazi, hivyo kuchangia katika utunzaji wa mazingira.

**Swali la 23**: Jando na unyago ni miongoni mwa tamaduni za zamani sana nchini Tanzania. Upi ni umuhimu wake kwa wanajamii husika?

A Iliwafanya waenende kama wageni
B Iliwazuia kupata elimu ya kigeni
C Iliwafanya wawadharau wageni
D Iliwafanya kupenda kazi na kujitegemea
E Ilikuza utamaduni wa kuwapenda wageni

Swali lilimtaka mtahiniwa kubaini umuhimu wa Jando na Unyago ambao ni moja kati ya tamaduni za zamani nchini Tanzania. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa wa wastani ambapo watahiniwa 627,896 (46.48%) walichagua jibu sahihi *D, Iliwafanya kupenda kazi na kujitegemea*. Watahiniwa hao walikuwa na umahiri wa kutosha kuhusu umuhimu wa Jando na Unyago katika jamii. Wakati wa jando na unyago, vijana wa kike na kiume waliandaliwa na kufundishwa na wazee kuwa wawajibikaji katika familia, jamii na taifa kwa ujumla, kufanya kazi za kujitegemea na kuwafanya kuwa na maadili mema.

Uchambuzi zaidi ulionesha kuwa, watahiniwa 701,803 (51.96%) waliochagua vipotoshi *A, Iliwafanya waenende kama wageni, B, Iliwazuia kupata elimu ya kigeni, C, Iliwafanya wawazarau wageni* na *E, Ilikuza utamaduni wa kuwapenda wageni* hawakuwa na umahiri kuwa, jando na unyago haikuanzishwa kwa lengo la kuwa na matokeo hasi kama ialivyobainishwa katika vipotoshi husika. Aidha, kipotoshi E, kilihusisha kuwapenda wageni, jambo ambalo si sahihi kwani jando na unyago vilifundisha kuwapenda na kuwaheshimu binadamu bila kubagua aina ya watu.

**Swali la 24**: Kaka yangu alipokwenda kulipa mahari kijiji cha Luponde, alielezwa kuwa ni lazima apeleke mbuzi, mkuki na jembe. Je vitu hivi vinawakilisha jambo lipi?

A Miiko B Mila C Desturi
D Michezo E Sanaa

Swali lilimtaka mtahiniwa kutambua jambo linalowakilishwa na vitu vitolewavyo katika mahari. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili

ulikuwa wa wastani kwani watahiniwa 775,223 (57.39%) walichagua jibu sahihi *B, Mila*. Watahiniwa hao waliweza kutambua kuwa mila ni sheria na kanuni zinazoongoza na zinazopaswa kufuatwa na jamii husika. Watahiniwa hao walionesha umahiri wao katika kubaini vitendo mbalimbali vinavyofanyika katika jamii, ambapo watu hutoa vitu kama sehemu ya mahari. Jambo hili liliwafanya kuelewa kuwa matendo hayo ni sehemu ya mila zinazotekelezwa na wanajamii.

Watahiniwa 126,909 (9.40%) waliochagua kipotoshi *A, Miiko*, hawakutambua kuwa miiko ni onyo au katazo linalowekwa na jamii husika. Kwa mfano, kwa jamii nyingi za Tanzania, ni mwiko kwa kaka kumuoa dada yake au mtoto wa kiume kumuoa mama yake. Sambamba hilo, watahiniwa 286,275 (21.19%) walichagua kipotoshi *C, Desturi*. Watahiniwa hao hawakuelewa kuwa desturi ni mienendo au namna ya kufanya mambo yaliyozoeleka katika jamii. Pia, watahiniwa 56,340 (4.17%) waliochagua kipotoshi *D, Michezo*, hawakujua kuwa michezo ni mazoezi mbalimbali ya viungo. Kwa mfano, mchezo wa mpira wa miguu, mchezo wa mpira wa mikono na mchezo wa riadha. Hivyo, michezo haihusiani kabisa na mila. Kwa kuongezea, watahiniwa 89,353 (6.61%) waliochagua kipotoshi *E, Sanaa*, hawakuwa na umahiri wa kuwawezesha kutofautisha mila na sanaa. Sanaa ni kufanya kitu kwa kutumia ufundi au ustadi ili kufikisha ujumbe au kufurahisha watu. Kwa mfano, sanaa ya nyimbo, muziki na ngoma. Kimsingi, watahiniwa waliochagua vipotoshi walidhihirisha uelewa finyu juu ya utamaduni na vielelezo vyake.

**Swali la 25**: Mwalimu aliwafundisha wanafunzi kuwa nchini Tanzania mtu anaweza kupata huduma zote kwa kupatana na wenyeji husika. Unafikiri ni jambo gani lililowezesha maelewano hayo?

A Uwepo wa lugha ya Kiingereza
B Uwepo wa lugha ya Kiswahili
C Matumizi ya lugha ya Kizaramo
D Matumizi ya lugha ya Kisukuma
E Uwepo wa lugha za Makabila

**Jedwali Na. 5: Idadi na asilimia ya ufaulu wa watahiniwa kwa kila chaguo**

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 78,919 | 964,922 | 61,109 | 61,389 | 167,711 | 16,724 |
| **Asilimia ya Watahiniwa** | 5.84 | 71.43 | 4.52 | 4.55 | 12.42 | 1.24 |

Swali lilimtaka mtahiniwa kubaini jambo linalomwezesha mtu kupata huduma zote kwa kupatana na wenyeji husika nchini Tanzania. Kama inavyooneshwa katika Jedwali Na. 5, ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa mzuri kwani watahiniwa 964,922 (71.43%) waliweza kuchagua jibu sahihi *B, Uwepo wa Lugha ya Kisw*ahili. Watahiniwa hao walielewa kuwa Lugha ya Kiswahili hutumika katika maeneo mengi nchini Tanzania kuanzia mijini hadi vijijini. Kiswahili kimekuwa ni lugha muhimu sana katika kuwaunganisha Watanzania. Lugha ya Kiswahili pia huwezesha mawasiliano baina ya watu, hivyo, hufanya mtu kuweza kupata huduma muhimu bila shida yoyote.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 78,919 (5.84%) waliochagua kipotoshi *A, Uwepo wa lugha ya Kiingereza*, hawakutambua kuwa Lugha ya Kiingereza siyo lugha ya taifa la Tanzania. Lengo la lugha ya Kingereza ni kuwasiliana kimataifa na katika biashara hasa zinazohusisha taifa la Tanzania na mataifa mengine. Aidha, lugha hiyo hutumika katika ufundishaji na ujifunzaji katika shule za msingi za mchepuo wa lugha ya Kiingereza na kama somo kwa shule zote za umma, Shule za Sekondari, Vyuo vya Kati na Vyuo Vikuu hapa nchini.

Zaidi ya hayo, watahiniwa 61,109 (4.52%) waliochagua kipotoshi *C, Matumizi ya lugha ya Kizaramo*, hawakutambua kuwa lugha ya Kizaramo inazungumzwa na wakazi wa baadhi ya maeneo hasa ya ukanda wa Pwani kama vile mikoa ya Dar es Salaam na Pwani. Pia, watahiniwa 61,389 (4.55%) waliochagua kipotoshi *D, Matumizi ya lugha ya Kisukuma*, hawakuwa na uelewa kuwa, lugha ya Kisukuma

ni lugha ya wenyeji wa mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Simiyu, Geita na Tabora.

Vilevile, watahiniwa 167,711 (12.42%) waliochagua kipotoshi *E, Uwepo wa lugha za Makabila*, hawakutambua kuwa lugha za makabila huzungumzwa na watu wa eneo moja na huwaleta pamoja watu ambao husikia lugha hizo. Hivyo, lugha za makabila zinafanya mawasiliano kati ya watu wa makabila tofauti kuwa magumu na huathiri upatikanaji wa huduma mbalimbali kwa wageni wanaofika katika maeneo hayo kutokana na kuzungumzwa katika eneo moja.

**Swali la 26**: Wanafunzi wa Darasa la Sita walitumia Barometa katika mafunzo kwa vitendo. Je, walikuwa wanapima kipengele kipi cha hali ya hewa?

A Mvua
B Jotoridi
C Unyevuanga
D Mgandamizo wa hewa
E Mawingu


Swali lilimtaka mtahiniwa kubaini kipengele cha hali ya hewa kinachopimwa kwa kutumia Barometa. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa wastani kwa sababu watahiniwa 684,396 (50.67%) ndio waliochagua jibu sahihi *D, Mgandamizo wa hewa*. Uchaguzi wa jibu hili unaonesha kuwa, watahiniwa hao waliweza kubainisha vipengele vya hali ya hewa na vifaa vinavyotumika kupimia vipengele hivyo.

Kwa upande mwingine, jumla ya watahiniwa 646,283 (47.84%) walichagua vipotoshi *A, Mvua, B, Jotoridi, C, Unyevuanga* na *E, Mawingu*. Uchaguzi wa vipotoshi hivyo unathibitisha kuwa watahiniwa hawakuwa na uelewa wa kutosha wa vipengele vya hali ya hewa na vifaa vinachotumika kupima. Kwani, mvua hupimwa kwa kifaa kiitwacho kipima mvua, Jotoridi hupimwa kwa kipima joto, Unyevuanga hupimwa kwa Haigromita na mawingu hupimwa kwa Oktasi.

**Swali la 27**: Katika mafunzo kwa vitendo ya namna ya kupima vipengele vya hali ya hewa, Miza alitoa jibu lake kwa kutumia asilimia. Je, alikuwa anapima kipengele kipi cha hali ya hewa?

| | | | |
|---|---|---|---|
| A | Mgandamizo wa hewa | B | Jotoridi |
| C | Kiwango cha mvua | D | Unyevuanga |
| E | Mwanga wa jua | | |

Swali lilimtaka mtahiniwa kubaini kipengele cha hali ya hewa ambacho kipimio chake hutumia asilimia kama kizio. Kwa ujumla, ufaulu katika swali hili ulikuwa hafifu kwa sababu watahiniwa 1,092,391 (80.87%) walichagua vipotoshi. Miongoni mwao, watahiniwa 323,865 (23.98%) walichagua kipotoshi *A, Mgandamizo wa hewa*. Watahiniwa hawa hawakuelewa kuwa Mgandamizo wa hewa huwasilishwa au hurekodiwa katika kizio cha ujazo cha Milibaa. Watahiniwa wengine 335,318 (24.82%) walichagua kipotoshi *B, Jotoridi* ambacho hurekodiwa katika kizio cha Sentigredi au Farinaiti. Vilevile, watahiniwa 321,080 (23.77%) walichagua kipotoshi *C, Kiwango cha mvua*. Jibu hili halikuwa sahihi kwa sababu kiwango cha mvua huwasilishwa katika kizio cha ujazo cha Milimita. Watahiniwa wengine, 112,128 (8.30%) walichagua kipotoshi *E, Mwanga wa jua* ambacho hurekodiwa kwa Saa na Dakika. Kwa ujumla, watahiniwa waliochagua vipotoshi walishindwa kutofautisha vipengele vya hali ya hewa, vifaa vya kupimia vipengele hivyo na vizio vinavyotumika kuwasilisha majibu ya vipimo hivyo. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili umeoneshwa katika Chati Na. 7.




**Chati Na. 7**: *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 27*

Pamoja na watahiniwa wengi kuchagua vipotoshi, watahiniwa 236,155 (17.48%) walichagua jibu sahihi *D, Unyevuanga*. Watahiniwa hao walikuwa mahiri katika vipengele vya hali ya hewa, vifaa vinavyotumika kupima na vizio vinavyotumika. Pia, uchaguzi wa jibu sahihi unaonesha kuwa watahiniwa walijifunza namna ya kupima na kurekodi vipengele vya hali ya hewa kwa kutumia vizio sahihi. Aidha umahiri huu huhusisha kufanyika kwa ziara ili kuona na kujifunza namna ambavyo vipengele vya hali ya hewa vinapimwa na kurekodiwa kwa kutumia vizio vyake, jambo ambalo huenda limesaidia uelewa huo.

**Swali la 28**: Upepo ni hewa inayovuma kwa kasi kutoka kanda zenye mgandamizo mkubwa wa hewa kuelekea kanda zenye mgandamizo mdogo. Ipi ni hasara inayosababishwa na hewa hiyo?

A Kupooza joto
B Kusababisha mvua
C Kukausha nguo
D Kuchavusha maua
E Kusambaza magonjwa

Swali lilimtaka mtahiniwa kubainisha hasara inayosababishwa na hewa inayotembea. Ufaulu katika swali hili ulikuwa wa wastani kwa kuwa watahiniwa 776,576 (57.49%) walichagua jibu sahihi *E, Kusambaza magonjwa*. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa kuhusu faida zitokanazo na upepo kama vile kuendesha mashine,

kusafirisha bidhaa (kwa kutumia jahazi), kuzalisha umeme na hasara kama vile kuezua paa la nyumba, kuangusha miti na kusambaza magonjwa. Magonjwa yanayoweza kusambazwa na upepo ni pamoja na Kifua kikuu, Corona na mafua.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 559,047 (41.39%) walichagua vipotoshi *A, Kupooza joto; B, Kusababisha mvua; C, Kukausha nguo na D, Kuchavusha maua*. Watahiniwa hao hawakuwa na umahiri kuhusu upepo na hasara zinazoweza kusababishwa nao. Vipotoshi vyote vinahusu faida za upepo. Kwa mfano, kipotoshi *A, Kupooza joto* kilichaguliwa na watahiniwa 212,364 (15.72%). Hii siyo hasara kwani jua linapowaka juu ya uso wa Dunia, hewa hupata joto na kuwa nyepesi. Hivyo hubeba unyevunyevu na kupaa angani. Hewa hii inavyozidi kupaa joto kali kwenye uso wa Dunia hupungua. Vilevile wakati wa joto, watu hutumia pangaboi ambalo hupuliza upepo kupooza mwili, kwani joto kali husababisha madhara ya kiafya.

**Swali la 29**: Mwalimu wa Darasa la Nne aliwataka wanafunzi wataje kifaa cha kupima hali ya hewa ambacho kipimio chake huweza kurekodiwa kwa vizio viwili tofauti. Je, wangetoa jibu lipi?

A Baromita  B Haigromita
C Anemomita  D Kipima mwanga wa jua
E Kipimajoto


Swali lilimtaka mtahiniwa kubainisha kifaa cha kupima hali ya hewa ambacho hurekodiwa kwa vizio viwili tofauti. Kwa ujumla, ufaulu katika swali hili ulikuwa hafifu, kwani watahiniwa 1,082,744 (80.16%) walichagua vipotoshi *A, Baromita; B, Haigromita; C, Anemomita* na *D, Kipima mwanga wa jua*. Watahiniwa hao hawakuwa na umahiri kuhusu vipimio na vizio vinavyotumika. Vipimio vyote vinavyotajwa kwenye vipotoshi hurekodiwa kwa kizio kimoja tu kila kimoja. Kwa mfano, Baromita hutumia kizio cha ujazo cha Milibaa, Haigromita hutumia Asilimia, Anemomita hutumia Kilomita kwa saa na mwanga wa jua hurekodiwa kwa muda (Saa na Dakika).

Kwa upande mwingine, watahiniwa 249,191 (18.45%) walichagua jibu sahihi *E, Kipima joto*. Uchaguzi wa jibu hili ulionesha kuwa watahiniwa hao walikuwa na uelewa mzuri wa vipengele vya hali ya hewa, vifaa vya kupimia na vizio vinavyotumika kwa kila kipengele cha hali ya hewa. Watahiniwa hawa walionesha kuwa walijifunza namna ambavyo vipengele vya hali ya hewa hupimwa na kurekodiwa. Aidha, kipima joto ndicho kipimio pekee ambacho huweza kurekodiwa kwa kutumia vizio viwili tofauti ambavyo ni Sentigredi na Fareniheiti, ikilinganishwa ni vipimio vingine vilivyobainishwa katika chaguzi.

**Swali la 30**: Mwalimu aliwafundisha wanafunzi wa Darasa la Sita juu ya zana za mawe za kale. Wanafunzi hao walipenda kujua zaidi kuhusu zana hizo. Je utawashauri kutembelea eneo gani la kihistoria ili waweze kuziona zana hizo?

A Kilwa Kisiwani B Amboni C Engaruka
D Isimila E Olduvai Gorge

Swali lilimtaka mtahiniwa kubaini eneo la kihistoria ambalo zana za mawe za kale zinapatikana. Kwa ujumla, ufaulu katika swali hili ulikuwa hafifu kwani watahiniwa 940,726 (69.65%) walichagua vipotoshi. Kati yao, watahiniwa 92,190 (6.82%) walichagua kipotoshi *A, Kilwa Kisiwani*. Jibu hili halikuwa sahihi kwa sababu Kilwa Kisiwani inahusisha mabaki ya majengo ya kale yaliyojengwa na Waarabu ikiwemo misikiti. Pia utamaduni wa Waarabu unajionesha kwenye ujenzi wa nyumba zinazopatikana katika eneo hilo. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hilo umeoneshwa katika Chati Na. 8.



**Chati Na. 8**: *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 30*

Aidha, watahiniwa 146,925 (10.88%) waliochagua kipotoshi *B, Amboni,* hawakuelewa kuwa eneo hili ni maarufu katika historia ya Tanzania kwa kuwa na mapango makubwa yenye maumbo mbalimbali na siyo zana za mawe za kale. Vivyo hivyo, watahiniwa wengine, 340,733 (25.23%) waliochagua kipotoshi *C, Engaruka*, hawakuelewa kuwa hilo ni eneo maarufu kwa mabaki ya masalia ya mifumo ya kilimo cha umwagiliaji iliyotumiwa na watu wa kale. Watahiniwa 360,693 (26.72%) waliochagua kipotoshi *E, Olduvai Gorge* pia hawakuwa sahihi. Olduvai Gorge ni eneo ambalo masalia ya fuvu la binadamu wa kale zaidi duniani lililogunduliwa na Dkt Louis Leakey na mkewe Dkt Mary Leakey mwaka 1959. Kwa ujumla, uchaguzi wa vipotoshi hivyo ni jambo lililoonesha kuwa, watahiniwa hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu maeneo mbalimbali ya kihistoria na kumbukumbu zinazopatikana katika maeneo hayo.

Watahiniwa 389,693 (28.85%) walichagua jibu sahihi *D, Isimila*. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa mzuri wa maeneo yenye kumbukumbu za masalia ya zana za mawe za kale. Pamoja na kusoma dhana hii kwenye vitabu wakiwa shuleni, uelewa mzuri zaidi unaweza kuwa umechangiwa na kuwepo kwa matangazo ya maeneo hayo kupitia vyombo vya habari kama vile Runinga na Majarida.

**Swali la 31**: Mjeta alitaka kutembelea maeneo mawili ya kihistoria maarufu kwa biashara ya utumwa nchini Tanzania. Je, maeneo yapi ya kihistoria utamshauri kutembelea?

A Amboni na Kilwa
B Kaole na Kalenga
C Isimila na Amboni
D Kaole na Kilwa Kisiwani
E Kondoa-Irangi na Kilwa

Swali lilimtaka mtahiniwa kuainisha maeneo mawili ya kihistoria yaliyokuwa maarufu kwa biashara ya utumwa nchini Tanzania. Kwa ujumla, ufaulu katika swali hili ulikuwa hafifu kwani jumla ya watahiniwa 1,008,512 (74.66%) walichagua vipotoshi *A, Amboni na Kilwa; B, Kaole na Kalenga; C, Isimila na Amboni* na *E, Kondoa – Irangi na Kilwa*. Watahiniwa hawakuweza kutofautisha maeneo mbalimbali na kumbukumbu za kihistoria zinazopatikana katika maeneo hayo. Hawakufahamu kuwa; Amboni ni eneo maarufu kwa kuwa na mapango makubwa yenye maumbo mbalimbali; Kilwa ulikuwa ni mji wa kibiashara hasa biashara ya kubadilishana bidhaa, mji wa utamaduni wa Kiswahili, biashara ya utumwa na kituo cha kunyongea watumwa waliokuwa wakaidi kusafirishwa. Vilevile, Kaole ni eneo lenye kumbukumbu za mabaki ya masalia ya majengo ya misikiti na vitu vya thamani vilivyoletwa na kutumiwa na wafanyabiashara kutoka Mashariki ya Mbali na eneo lililofanyika biashara ya utumwa. Kalenga ni eneo lililopo mkoa wa Iringa lenye kumbukumbu za mabaki ya silaha za jadi zilizotumika wakati wa ukoloni wa Mjerumani pamoja na fuvu la Mkwawa. Isimila ni eneo lenye kumbukumbu za masalia ya zana za mawe za kale au mwanzo na pia, Kondoa – Irangi ni eneo ambalo lina michoro mbalimbali ya mapangoni iliyochorwa katika miamba.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 322,344 (28.86%) walichagua jibu sahihi *D, Kaole na Kilwa Kisiwani.* Watahiniwa hao walionesha kuwa na uelewa mzuri wa maeneo ya kihistoria yaliyokuwa vituo vya biashara ya utumwa nchini Tanzania.

**Swali la 32**: Kwa nini Bagamoyo ni mji maarufu wa kihistoria nchini Tanzania?

A Unatunza masalia ya binadamu wa kale
B Unatunza mifumo ya umwagiliaji ya kale
C Ni eneo la vita vya kikoloni katika Tanzania
D Ni eneo la ustaarabu wa kale katika Tanzania
E Ni eneo la biashara ya utumwa na ustaarabu wa Kiarabu

Swali lilimtaka mtahiniwa kutoa sababu zinazofanya Bagamoyo kuwa mji maarufu wa kihistoria nchini Tanzania. Ufaulu katika swali hili ulikuwa wa wastani kwani watahiniwa 580,421 (42.97%) walichagua jibu sahihi *E, Ni eneo la biashara ya utumwa na ustaarabu wa Kiarabu*. Watahiniwa hao walionesha uelewa mzuri wa maeneo ambayo yalikuwa kitovu cha Biashara ya utumwa ikiwemo Bagamoyo. Aidha, mji wa Bagamoyo ulikuwa kitovu cha usafirishaji wa watumwa kutokana na kuwa katika Pwani ya Bahari ya Hindi. Hivyo watumwa walifanyiwa ukaguzi katika eneo hilo, kufungwa kwenye minyororo kisha kusafirishwa kwenda Zanzibar na nchi za Kiarabu kama vile Oman. Watumwa walitumika kufanya kazi za ndani na uzalishaji mali katika mashamba. Pia, kuhamishia makazi ya kisultani kutoka Maskat hadi Stone town Unguja kulikofanywa na Sultan Said bin Sultan (Sayyid Said) mwaka 1840) kulifanya eneo la Bagamoyo kuwa na ustaarabu wa Kiarabu, kwani Sutan aliendesha shughuli zake katika eneo hilo.

Kwa upande mwingine, jumla ya watahiniwa 750,580 (55.57%) walichagua vipotoshi *A, Unatunza masalia ya binadamu wa kale; B, Unatunza mifumo ya umwagiliaji ya kale; C, Ni eneo la vita vya kikoloni nchini Tanzania na D, Ni eneo la ustaarabu wa kale katika Tanzania*. Watahiniwa hao hawakuweza kutofautisha maeneo mbalimbali ya kihistoria na kumbukumbu za kihistoria zinazopatikana katika maeneo hayo. Hawakuelewa kuwa kumbukumbu za kihistoria za masalia ya binadamu wa kale yanatunzwa Olduvai Gorge; kumbukumbu za masalia ya mifumo ya kilimo cha umwagiliaji iliyotumika na watu wa kale ziko Engaruka; maeneo ya vita vya kikoloni nchini Tanzania ni Iringa ambapo Mkwawa alipigana na Wajerumani; na eneo la ustaarabu wa kale

katika Tanzania ni Iringa katika mawe ya Gangilonga na Kondoa Irangi katika mkoa wa Dodoma ambayo yanaonesha masalia ya michoro ya watu wa kale.

**Swali la 33**: Wakati wa kipindi kinachohusu majanga mbalimbali, mwanafunzi mmoja aliuliza kuhusu faida ya mlipuko wa volkano kwa binadamu. Lipi kati ya yafuatayo lingekuwa jibu lako?

A Husababisha kutokea kwa moto
B Husababisha kutokea kwa chemichemi za maji
C Husababisha kutokea kwa moshi mzito
D Husababisha kutokea kwa mawe makubwa
E Husababisha kuporomoka kwa ardhi

Swali lilimtaka mtahiniwa kubainisha faida ya mlipuko wa volkano kwa binadamu. Kwa ujumla, ufaulu katika swali hili ulikuwa wa wastani kwani watahiniwa 592,713 (43.88%) walichagua jibu sahihi *B, Husababisha kutokea kwa chemichemi za maji*. Watahiniwa hao walionesha kuwa na uelewa mzuri wa faida na hasara zinazotokana na mlipuko wa volkano kwa binadamu.

Kwa upande mwingine, jumla ya watahiniwa 739,648 (54.76%) walichagua vipotoshi *A, Husababisha kutokea kwa moto; C, Husababisha kutokea kwa moshi mzito; D, Husababisha kutokea kwa mawe makubwa na E, Husababisha kuporomoka kwa ardhi.* Watahiniwa hawa walishindwa kutofautisha athari chanya na hasi za mlipuko wa volkano. Hawakuelewa kuwa kutokea kwa moto, kutokea kwa moshi mzito, kutokea kwa mawe makubwa na kusababisha kuporomoka kwa ardhi ni madhara kwa binadamu na kwa mazingira kwa ujumla.

**Swali la 34**: Janga la moto wa asili husababisha hasara kubwa kwa watu na taifa kwa ujumla. Kipi ni chanzo kikuu cha janga hilo?

A Mlipuko wa volkano B Radi C Urinaji asali
D Uwindaji E Upishi

Swali lilimtaka mtahiniwa kubainisha chanzo kikuu cha janga la moto wa asili. Ufaulu katika swali hilo ulikuwa hafifu kwani jumla ya watahiniwa 1,065,071 (78.85%) walichagua vipotoshi *C, Urinaji asali; D, Uwindaji, pamoja na E, Upishi*. Watahiniwa hao hawakuwa na uelewa kuwa hivyo vyote siyo vyanzo vya asili, bali ni vyanzo vinavyosababishwa na shughuli za binadamu.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 268,775 (19.90%) walichagua jibu sahihi *B, Radi*. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu majanga ya moto. Waliweza pia kutofautisha majanga ya moto wa asili na yale yanayosababishwa na mwanadamu, pamoja na vyanzo vyake. Radi ni janga la asili kwa sababu asili yake ni volteji inayojijenga kati ya mawingu angani yenye chaji tofauti au pia kati ya mawingu na ardhi. Aidha, radi husababisha janga la moto kwani chaji hiyo husababisha kutokea kwa cheche ambazo huunguza majani au miti, hivyo husababisha moto.

**Swali la 35**: Unaweza ukatoa ushauri upi kwa wanakijiji ambao hutumia kuni kama nishati katika maisha yao ya kila siku?

A Kukata kuni asubuhi na mapema kabla ya jua kuwaka
B Kutengeneza mkaa kwa kutumia mabaki ya mazao
C Kutumia vizuri miti iliyokatwa
D Uwepo wa watu maalum wa kuuza kuni
E Kukata kuni mbali na maeneo yao ya kuishi

**Jedwali Na. 6: Idadi na asilimia ya ufaulu wa watahiniwa kwa kila chaguo**

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya Watahiniwa** | 105,337 | 390,594 | 328,253 | 101,739 | 405,603 | 19,248 |
| **Asilimia ya Watahiniwa** | 7.80 | 28.92 | 24.30 | 7.53 | 30.03 | 1.42 |

Swali lilimtaka mtahiniwa kubainisha ushauri mzuri kwa wanakijiji ambao hutumia mkaa kama nishati. Kama Jedwali Na. 6

linavyoonesha, ufaulu katika swali hilo ulikuwa hafifu kwani jumla ya watahiniwa 940,932 (69.66%) walichagua vipotoshi *A, Kukata miti asubuhi na mapema kabla ya jua kuwaka; C, Kutumia vizuri miti iliyokatwa; D, Uwepo wa watu maalum wa kuuza kuni na E, Kukata kuni mbali na maeneo yao ya kuishi*. Watahiniwa hao hawakuwa na uelewa wa kutosha kubaini kuwa kukata miti huathiri mazingira bila kujali muda au sababu ya kukata miti hiyo.


Kwa upande mwingine, watahiniwa 390,594 (28.92%) walichagua jibu sahihi *B, Kutengeneza mkaa kwa kutumia mabaki ya mazao*. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa mzuri kuhusu dhana ya utunzaji wa mazingira kwa kutumia nishati mbadala. Mabaki ya mazao yakiwekwa kwenye tanuru kisha kuchomwa na baadae kuweka kwenye mashine maalum hutengeneza vipande vya mkaa ambao ni sawa na mkaa unaopatikana kwa kuchoma miti. Mkaa unaotengenezwa kwa mabaki ya mimea ya mazao huwa bora zaidi kwani hautoi moshi wakati wa kuutumia. Hivyo, watahiniwa hao walielewa madhara ya kutumia kuni kama chanzo cha nishati katika mazingira kuwa husababisha kutoweka kwa misitu.

**Swali la 36**: Kwanini unashauriwa kunyunyizia maji kiasi kwenye nguo zilizokauka sana kabla ya kuzipiga pasi?

A Kuondoa vumbi au uchafu
B Kuondoa mikunjo kwa urahisi
C Kuepuka kuunguza nguo
D Kuua vimelea vya magonjwa
E Kuepuka nguo kupauka

Swali lilimtaka mtahiniwa kubainisha sababu za kunyunyizia maji kiasi kwenye nguo zilizokauka sana kabla ya kuzipiga pasi. Ufaulu katika swali hili ulikuwa hafifu kwani kati ya watahiniwa 1,350,774 waliofanya swali hilo, watahiniwa 1,035,585 (76.74%) walichagua vipotoshi. Kati yao, watahiniwa 81,875 (6.06%) walichagua kipotoshi *A, Kuondoa vumbi na uchafu*. Jibu hili halikuwa sahihi kwa kuwa vumbi na uchafu katika nguo huondolewa kwa kuzifua. Aidha, watahiniwa 719,436 (53.26%) waliochagua kipotoshi *C, Kuepuka kuunguza nguo*, hawakuelewa kuwa kupunguza moto wakati wa kupiga pasi huepusha kuunguza nguo. Zaidi ya hayo, watahiniwa

92,946 (6.88%) walichagua kipotoshi *D, Kuua vimelea vya magonjwa.* Watahiniwa hawa hawakuwa sahihi kwa sababu vimelea vya magonjwa kwenye nguo, vinaweza kuondolewa kwa kupiga pasi bila hata kunyunyizia maji kwa kuwa joto la pasi huviua. Vilevile, watahiniwa 142,328 (10.54%) waliochagua kipotoshi *E, Kuepuka nguo kupauka,* walishindwa kutambua kuwa nguo inaponyunyiziwa maji haipauki. Upaukaji wa nguo hutokana na nguo kufuliwa mara kwa mara au kuachwa juani kwa muda mrefu. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hilo umeoneshwa katika Chati Na. 9.





**Chati Na. 9**: *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 36*

Kwa upande mwingine, watahiniwa 297,142 (22.00%) walichagua jibu sahihi *B, Kuondoa mikunjo kwa urahisi*. Watahiniwa hao walionesha uelewa kuhusu dhana ya usafi wa mavazi na mwili. Maji ya kiasi yanapowekwa kwenye nguo iliyokauka sana husaidia kulainisha nyuzi za nguo husika na hivyo inapopigwa pasi mikunjo huondoka kwa urahisi.

**Swali la 37**: Madoa yanapoingia kwenye nguo husababisha nguo kuwa na mwonekano mbaya. Je, unaweza kutumia kitoa madoa kipi kuondoa madoa yaliyosababishwa na damu?

A Maji yaliyochanganywa na limao
B Maji baridi yaliyochanganywa na chumvi
C Maziwa ya mgando
D Maji moto yaliyochanganywa na chumvi
E Mionzi ya Jua

Swali lilimtaka mtahiniwa kubaini aina ya kitoa madoa kinachofaa kutoa madoa kwenye nguo yaliyosababishwa na damu. Ufaulu katika swali hili ulikuwa hafifu kwani kati ya watahiniwa 1,350,774 waliofanya swali hilo, watahiniwa 1,106,882 (81.93%) walichagua vipotoshi *A, Maji yaliyochanganywa na limau; C, Maziwa ya mgando; D, Maji moto yaliyochanganywa na chumvi na E, Mionzi ya jua*. Watahiniwa hao hawakuelewa kuwa chumvi, maji ya moto, limao, maziwa mgando na mionzi ya jua hutumika kuondoa madoa yanayotokana na vyakula kama matunda na mchuzi. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hilo umeoneshwa katika Chati Na. 10.




**Chati Na. 10**: Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 37


Hata hivyo, watahiniwa 226,576 (16.77%) walichagua jibu sahihi *B, Maji baridi yaliyochanganywa na chumvi*. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa kuwa chumvi inapochanganywa na maji hutengeneza

mchanganyiko. Hivyo, mchanganyiko huo unapotumika kufua nguo yenye madoa ya damu hufyonza madoa hayo na hivyo huifanya nguo kuwa safi.

**Swali la 38**: Shamte aliomba ushauri wa vyakula vitakavyomsaidia kupambana na magonjwa. Je, ungemshauri kutumia vyakula gani?

A Mboga za majani na matunda
B Mchele na ndizi
C Nyama na kumbikumbi
D Samaki na maharage
E Mahindi na viazi

Swali lilimtaka mtahiniwa kutoa ushauri wa vyakula vinavyosaidia kupambana na magonjwa. Ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwani kati ya watahiniwa 1,350,774, watahiniwa 1,121,363 (83.02%) walichagua jibu sahihi *A, Mboga za majani na matunda*. Uelewa wa watahiniwa hao umetokana na kuwa na elimu juu ya mlo kamili, unaojumuisha vyakula vya mbogamboga, matunda, wanga, vitamini, protini na mafuta na kazi zake. Aidha, walielewa kuwa mboga za majani na matunda husaidia kupambana na magonjwa kwani vina Potassium, Vitamin A na C ambazo husaidia mwili kupambana na magonjwa. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hilii umeoneshwa katika Chati Na. 11.




**Chati Na. 11**: *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 38*

Jumla ya watahiniwa 216,321 (16.01%) walichagua vipotoshi *B, Mchele na Ndizi, C, Nyama na Kumbikumbi, D, Samaki na Maharage* na *E, Mahindi na viazi*. Watahiniwa hao hawakuelewa kuwa, mchele, ndizi, mahindi na viazi ni vyakula vya wanga na vina kazi ya kuupa mwili nguvu; ilihali nyama, kumbikumbi, samaki na maharage ni vyakula vya protini vinavyojenga mwili. Uchaguzi wa vipotoshi hivyo unaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu aina za vyakula na kazi zake katika mwili wa binadamu.

**Swali la 39**: Sanaa husaidia kupata vitu mbalimbali kwa ajili ya matumizi mbalimbali. Je ni vifaa vipi vinatokana na sanaa ya ususi?

A Mikeka, kata za mezani na vikapu
B Vikapu, kata za mezani na vyungu
C Kata za mezani, vyungu na mikeka
D Mikeka, kofia na sufuria
E Sufuria, kata ya mezani na vikapu

Swali lilimtaka mtahiniwa kutambua aina ya vifaa vinavyotokana na sanaa ya ususi. Ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwani watahiniwa 1,007,492 (74.59%) walichagua jibu sahihi *A, Mikeka, kata za mezani na vikapu.* Hii ni kwa sababu walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu sanaa ya ususi. Watahiniwa hao walielewa kuwa, mikeka, kata za mezani na vikapu ni vitu vinavyosukwa kwa kutumia malighafi kama vile ukili, kamba na makuti.

Hata hivyo, jumla ya watahiniwa 329,637 (24.40%) walivutiwa na vipotoshi*; B, Vikapu, kata za mezani na vyungu; C, Kata za mezani, vyungu na mikeka; D, Mikeka, kofia na sufuria na E, Sufuria, kata ya mezani na vikapu*. Vipotoshi hivyo havikuwa sahihi kutokana na uwepo wa vyungu na sufuria ambapo, vyungu vinatokana na sanaa ya ufinyanzi na sufuria inatengenezwa kwa kutumia madini ya chuma au bati. Uchaguzi wa vipotoshi hivyo unaonesha kuwa, watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kutofautisha sanaa ya ususi na sanaa nyingine kama vile ufinyanzi, uchongaji na udarizi.

**Swali la 40** : Kwanini ni muhimu kusoma tarehe ya mwisho ya matumizi ya bidhaa kabla ya kununua?

A Kulinda afya ya muuzaji
B Kupata bidhaa halisi
C Kulinda afya ya mtumiaji
D Kupata bidhaa mpya
E Kumlinda mtengenezaji


Swali lilimtaka mtahiniwa kubaini umuhimu wa kusoma tarehe ya mwisho ya matumizi ya bidhaa kabla ya kununua. Ufaulu katika swali hili ulikuwa wa wastani kwani watahiniwa 668,370 (49.48%) walichagua jibu sahihi *C, Kulinda afya ya mtumiaji*. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha kubaini athari za kiafya zinazotokana na matumizi ya bidhaa zilizopita muda wake wa matumizi. Pia, walielewa kuwa ni hatari kwa mlaji au mtumiaji kutumia bidhaa iliyoisha muda wa matumizi yake kwani huweza kuleta madhara katika afya kama vile kizunguzungu, kichefuchefu, kuharisha, kunguruma kwa tumbo na hata kuweza kusababisha vifo.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 68,742 (5.09%) walichagua kipotoshi *A, Kulinda afya ya muuzaji*. Watahiniwa hao hawakuelewa kuwa muuzaji jukumu lake kubwa ni kuuza bidhaa kwa mtumiaji, hivyo mara nyingi hahusiki moja kwa moja kutumia bidhaa husika. Hivyo, ikiwa bidhaa imepitwa na wakati, anayeathirika ni mtumiaji. Vilevile, watahiniwa wengine 331,350 (24.53%) waliochagua kipotoshi *B, Kupata bidhaa halisi*, hawakuelewa kuwa bidhaa halisi na zenye ubora huthibitishwa na Shirika la Viwango Tanzania (Tanzania Bureau of Standards - TBS) kwa kuwekwa alama ya ubora ya TBS na siyo tarehe ya mwisho ya matumizi. Vilevile, watahiniwa 206,133 (15.26%) waliochagua kipotoshi *D, Kupata bidhaa mpya*, hawakuelewa kuwa bidhaa mpya ni ile ambayo haikuwepo kwenye akiba ya muuzaji. Zaidi ya hayo, watahiniwa 58,939 (4.36%) waliochagua kipotoshi *E, Kumlinda mtengenezaji*, hawakuelewa kuwa, mtengenezaji ndiye anayechakata bidhaa ikiwa bado mpya kabisa na ikishakamilika huweka tarehe ya mwisho ya matumizi. Kwa hiyo, uchaguzi wa vipotoshi hivyo unaonesha kuwa, watahiniwa hao hawakuwa na umahiri wa kutosha kubaini athari za kutumia bidhaa zilizopita muda wake wa matumizi.

## 2.2 Sehemu B: Maswali ya Majibu Mafupi


**Swali la 41:** Ubunifu unamsaidiaje mjasiriamali katika shughuli zake? Toa hoja mbili.

Swali lilimtaka mtahiniwa kutoa hoja mbili kuonesha namna ubunifu unavyomsaidia mjasiriamali katika shughuli zake. Kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri kwani, watahiniwa 442,853 (32.79%) walipata alama zote 02, watahiniwa 427,881 (31.69%) walipata alama 01 na watahiniwa 479,618 (35.52%) walipata 00. Chati Na. 12 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.




**Chati Na. 12:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 41*

Jumla ya watahiniwa 442,853 (32.79%) walipata alama 02 kwa sababu walitoa hoja zote mbili kwa usahihi. Hoja walizotoa ni pamoja na: *husaidia kuboresha bidhaa au huduma, Husaidia kuongeza faida, Husaidia kuthibiti wizi* na *Husaidia kuhimili ushindani*. Usahihi wa majibu hayo unaonesha kuwa, watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu faida za ubunifu katika biashara. Kielelezo Na. 1:1 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi kutoka kwa mtahiniwa mwenye ujuzi na maarifa ya kutosha katika swali hili.


SWALI LA 41

Hoja mbili kuhusu ubunifu unavyomsaidia mjasiriamali katika shughuli zake ni:-
a) Kuwavutia wateja kwa mbinu yake mpya aliyobuni
b) Kumuongezea kipato kwa ubunifu mpya (kwa mfano kagundua bidhaa nyingine bora zaidi atawapenya watu kuvutiwa na bidhaa hiyo na kuinunua kwa wingi kwa hiyo atapata kipato)


**Kielelezo Na. 1.1:** *Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 41*

Kama inavyoonekana katika kielelezo 1.1, mtahiniwa alitoa majibu mawili sahihi. Katika sehemu ya kwanza mtahiniwa alieleza kuwa ubunifu unamsaidia mjasiriamali kuwavutia wateja. Katika sehemu ya pili mtahiniwa alieleza kuwa ubunifu unamsaidia kuongeza kipato kwani watu huvutiwa na bidhaa zake hivyo kununua kwa wingi.

Vilevile, watahiniwa 427,881 (31.69%) walipata alama 01 katika swali hili kwani walitoa hoja moja sahihi na nyingine isiyo sahihi. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya wastani kuhusu faida ya ubunifu kwa mjasiriamali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika, *kuvutia wateja* na *uthubutu*. Mtahiniwa huyu alishindwa kutambua kwamba *uthubutu* ni sifa ya mjasiriamali na siyo faida ya ubunifu, hivyo halikuwa jibu sahihi. Mtahiniwa mwingine aliandika *wajasiriamali kupoteza wateja* na *mjasiriamali kuongeza wateja.* Mtahiniwa huyu hakutambua kuwa *kupoteza wateja* ni matokeo ya kutokuwa mbunifu. Pia mtahiniwa mwingine aliandika *wajasiriamali kuongeza wateja* na *serikali kutunga sharia*. Mtahiniwa huyo hakutambua kuwa serikali kutunga sheria ni njia ya kudhibiti njia zisizo halali katika ujasiriamali.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 479,618 (35.52%) walipata 00. Watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu faida ya ubunifu katika biashara. Kwa mfano, baadhi ya watahiniwa walieleza sifa za mjasiriamali kama vile; *kuwa mwaminifu, kuwa* na *ubunifu na kuweza kutumia fursa vizuri*. Wengine walielezea njia zisizo halali katika ujasiriamali kama vile; *kujua muda bidhaa inapoweza kutumika na muda wa kuisha matumizi* na *kuuza bidhaa zisizo na ubora.* Zaidi ya hayo, watahiniwa wengine walielezea njia halali za ujasiriamali kama

vile; *kulipa kodi kwa wakati* na *kutoa elimu kwa jamii*. Kielelezo Na. 1.2 kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali hili.


SWALI LA 41


Kujua uzuri wa bidhaa
Kujua muda wa bidhaa inapo weza kutumika na muda wa kuisha matumizi

**Kielelezo Na. 1.2:** *Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 41*

Katika kielelezo Na. 1.2, mtahiniwa ameeleza mambo anayopaswa kufanya mteja kabla ya kununua bidhaa, badala ya kueleza faida ya ubunifu katika biashara.


**Swali la 42:** Wanafunzi walijadili kuhusu mistari ya kubuni inayochorwa kuanzia Kaskazini kuelekea Kusini ambayo hukutana kwenye ncha za Dunia. Yapi ni matumizi mawili ya mistari hiyo.

Swali lilimtaka mtahiniwa kutaja matumizi mawili ya mistari ya kubuni inayochorwa kuanzia Kaskazini kuelekea Kusini kwenye ncha za ramani ya Dunia. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa hafifu kwa sababu watahiniwa 227,350 (16.84%) walipata alama zote 02, watahiniwa 277,686 (20.56%) walipata alama 01 na watahiniwa wengine, 845,316 (62.60%) walipata 00. Chati Na. 13 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hilo.




**Chati Na. 13:** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 42*

Watahiniwa 845,316 (62.60%) walipata 00. Watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mistari ya Longitudo. Kwa mfano; baadhi ya watahiniwa waliandika, hatua za kutafuta muda kama vile; *kutafuta tofauti ya nyuzi* na *kutafuta tofauti ya muda.* Wengine walitoa maana ya mistari ya Latitudo na Longitudo kama vile; *latitudo ni mistari ya ulalo* na *longitudo ni mistari ya wima*. Pia, watahiniwa wengine waliandika sifa za ramani kama vile; *kuonesha ufunguo* na *kuonesha kichwa cha habari.* Kielelezo Na. 2.1 kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi kutoka kwa mtahiniwa.





**Kielelezo Na. 2.1:** *Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 42*

Katika Kielelezo Na. 2.1, mtahiniwa aliandika matokeo ya Dunia kulizunguka Jua, badala ya matumizi ya mistari ya Longitudo.

Hata hivyo, watahiniwa 277,686 (20.56%) walipata alama 01 katika swali hili kwa sababu walitoa hoja moja sahihi na moja isiyo sahihi au walitoa hoja moja tu sahihi. Hivyo, watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya wastani kuhusu mistari ya Longitudo. Kwa mfano; mtahiniwa aliandika, *husababisha majira ya mwaka* na *kupima eneo la Dunia.* Mtahiniwa huyo, hakutambua kuwa *majira ya mwaka* ni matokeo ya Dunia kulizunguka Jua. Pia, mwingine aliandika *kuonesha mahali fulani* na *kujua hali ya hewa.* Mtahiniwa huyo hakutambua kuwa kuna vifaa maalum ambavyo hutumika kupima vipengele vya hali ya hewa. Kwa mfano, jotoridi hupimwa na kipimajoto.

Watahiniwa 227,350 (16.84%) waliopata alama 02 waliweza kujibu swali kwa usahihi. Baadhi ya majibu ya watahiniwa katika kundi hili ni pamoja na; *kuonesha mahali au maeneo katika ramani, kukokotoa muda, kupima umbali katika ramani na kuongoza manahodha na marubani*, *kubaini siku na tarehe* na *kutafuta maeneo katika ramani*. Majibu hayo yalionyesha kuwa, watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mistari ya Longitudo na Latitudo. Kielelezo Na. 2.2 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi kutoka kwa mtahiniwa.


SWALI LA 42
i) Kutafuta muda wa mahali husika
ii) Kuonesha mahali husika


**Kielelezo Na. 2.2:** *Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 42*

**Swali la 43:** Mtaalamu wa hali ya hewa aliwataka wanafunzi kupima kiwango cha mgandamizo wa hewa kwa siku hiyo.

(a) Je, wanapaswa kutumia kifaa gani?

(b) Ni kizio kipi watatumia kuwasilisha taarifa hiyo?

Swali hili lilikuwa na sehemu mbili ambapo mtahiniwa alitakiwa (a) kutaja kifaa cha kupimia mgandamizo wa hali ya hewa na (b) kutaja kizio cha kuwasilisha mgandamizo wa hali ya hewa. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa wa wastani kwani watahiniwa 89,241 (6.61%) walipata alama zote 02, watahiniwa 626,906 (46.42%) walipata alama 01 na watahiniwa wengine, 634,205 (46.97%) walipata 00. Chati Na. 14 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hilo.




**Chati Na. 14:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika swali la 43*

Jumla ya watahiniwa 634,205 (46.97%) waliopata 00, hawakuwa na uelewa wa kuweza kubainisha vipengele vya hali ya hewa, vifaa vinavyotumika kupima na vizio vyake. Kwa mfano, baadhi ya watahiniwa waliandika *Kipima joto* katika sehemu (a) na *Sentigredi* katika sehemu (b). Watahiniwa hao walishindwa kutambua kwamba *Sentigredi* ni kizio cha *Jotoridi*. Watahiniwa wengine, waliandika *Hygromita* katika sehemu (a) na *Milimita* katika sehemu (b). Hawa pia, hawakutambua kuwa *Hygromita* hupima *Unyevuanga* na *Milimita* ni kizio kinachowasilisha kiwango cha *Mvua*. Kielelezo Na. 3.1 kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi kutoka kwa mtahiniwa.



SWALI LA 43 i) themo meta
ii) Asilimia

**Kielelezo Na. 3.1:** *Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 43*

Katika Kielelezo 3.1, mtahiniwa aliandika themometa ambalo ni jina la kifaa kinachotumika kupima joto na kizio cha asilimia ambacho sio kizio sahihi kwa kifaa hicho. Hivyo, mtahiniwa alishindwa kutambua vifaa vya kupima hali ya hewa na vizio vyake.

Pia, watahiniwa 626,906 (46.42%) walipata alama 01. Watahiniwa hao waliandika jibu sahihi moja na moja lisilo sahihi au waliandika jibu moja tu sahihi. Majibu yao yanaonesha kuwa watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya wastani kuweza kubaini vipengele vya hali ya hewa, vifaa vinavyotumika kupima na vizio vinavyotumika kurekodia. Mfano, mtahiniwa mmoja aliandika *Anemomita* katika sehemu (a) na *Milibaa* katika sehebu (b). Mtahiniwa huyu alishindwa kutofautisha *Barometa* na *Anemomita* kwa sababu, *Anemomita* hupima kasi ya upepo ambapo kizio chake ni *Kilomita kwa saa*. Mtahiniwa mwingine aliandika (a) Barometa na (b) Jotoridi. Huyu hakutambua kuwa *Jotoridi* hupimwa kwa *Kipimajoto* na kizio chake ni *Sentigredi* au *Farinaiti*. Pia, mtahiniwa mwingine aliandika (a) *Barometa* na *(b) Unyevuanga*. Naye pia hakutambua kuwa *unyevuanga* kizio chake ni asilimia.


Katika swali hili, watahiniwa 89,241 (6.61%) walipata alama 02 kwani waliandika majibu sahihi katika sehemu zote mbili. Watahiniwa hao waliandika *Barometa* katika sehemu (a) *na Milibaa katika sehemu* (b). Usahihi wa majibu hayo unaonesha kuwa, watahiniwa waliweza kubainisha vipengele vya hali ya hewa, vifaa vinavyotumika kupima na vizio vinavyotumika kurekodia. Kielelezo Na. 3.2 kinaonesha sampuli ya majibu sahihi kutoka kwa mtahiniwa.




**Kielelezo Na. 3.2:** *Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 43*

**Swali la 44:** Mafuriko ni miongoni mwa majanga ya asili yanayoleta madhara. Andika tahadhari mbili zinazoweza kuchukuliwa juu ya madhara yanayoweza kutokea.


Swali lilimtaka mtahiniwa kuandika tahadhari mbili zinazoweza kuchukuliwa dhidi ya madhara ya mafuriko kama janga la asili. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hilo ulikuwa wa wastani kwani watahiniwa 374,283 (27.72%) walipata alama zote 02, watahiniwa 278,631 (20.63%) walipata alama 01 na watahiniwa 697,438 (51.65%) walipata 00. Chati Na. 15 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.




**Chati Na. 15**: *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 44*

Watahiniwa 697,438 (51.65%) walipata 00 hawakuwa na ufahamu kabisa kuhusu majanga ya asili, madhara na tahadhari zinazopaswa kuchukuliwa ili kuepukana nayo. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja

aliandika *moto wa asili* na *volkano*. Mtahiniwa huyu alishindwa kutambua kwamba hayo ni majanga ya asili na siyo tahadhari za kukabiliana na majanga hayo. Mtahiniwa mwingine aliandika *mvua* na *unyevuanga*. Mtahiniwa huyu hakuelewa kuwa hivyo ni vipengele vya hali ya hewa na siyo tahadhari zinazopaswa kuchukuliwa ili kukabiliana na majanga ya asili. Pia, mwingine aliandika *mazao ya chakula (mahindi* na *viazi)* ambayo si tahadhari za kukabiliana na majanga ya asili. Watahiniwa hao wachache wametumika kuwakilisha wengine wengi wa namna hiyo. Kielelezo Na. 4.1 kinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi kutoka kwa moja ya mtahiniwa katika kundi hilo.





**Kielelezo Na. 4.1:** *Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 44*

Katika kielelezo Na. 4.1, mtahiniwa ameandika madhara yanayosababishwa na mafuriko, badala ya tahadhari za kuchukua ili kuepuka madhara yanayosababishwa na mafuriko.

Pia, watahiniwa 278,631 (20.63%) waliopata alama 01 kutokana na kuandika jibu moja sahihi na moja lisilo sahihi au waliandika jibu moja tu sahihi. Watahiniwa hao walikuwa na ufahamu wa wastani kuhusu majanga ya asili, madhara na tahadhari zinazopaswa kuchukuliwa ili kuepukana nayo. Kwa mfano; mtahiniwa mmoja aliandika *kutoishi mabondeni* na *kutumia ardhi vizuri.* Mtahiniwa huyu alishindwa kutambua kuwa *kutumia ardhi vizuri* ni jambo muhimu katika kulinda ardhi. Mtahiniwa mwingine aliandika *kuleta maafa* na *kutunza mazingira*. Mtahiniwa huyo hakutambua kuwa *kuleta maafa* ni athari za majanga ya asili na siyo njia ya kujikinga na majanga ya asili. Pia, mtahiniwa mwingine aliandika *kutoa elimu kwa jamii* na *kuharibu miundo mbinu.* Mtahiniwa huyu pia hakujua kuwa kuharibu miundo mbinu ni athari hasi za majanga ya asili na siyo njia ya kujikinga.


Jumla ya watahiniwa 374,283 (27.72%) walipata alama 02. Watahiniwa hao waliweza kuandika tahadhari mbili zinazoweza kuchukuliwa dhidi ya madhara ya mafuriko. Watahiniwa hao waliandika kati ya majibu yafuatayo; *kuepuka kuishi maeneo hatarishi, kuhakikisha mazingira yanakuwa masafi, kuwa na mipango miji endelevu, kupanda miti na nyasi* na *kutoa elimu kwa umma.* Hii inadhihrisha kuwa watahiniwa hawa walikuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu majanga ya asili, madhara na tahadhari zinazopaswa kuchukuliwa ili kuepukana nayo. Kielelezo Na. 4.2 kinaonesha sampuli ya majibu kutoka kwa mtahiniwa mwenye ujuzi na maarifa ya kutosha kuhusu athari za mafuriko.


SWALI LA 44 kupanda miti na nyasi
kukaa mbali na mabondo

**Kielelezo Na. 4.2:** *Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 44*

**Swali la 45:** Utamaduni ni uhai, utambulisho na tunu ya taifa inayorithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Je, mambo yapi mawili yanaathiri utamaduni wa jamii za Kitanzania?


Swali lilimtaka mtahiniwa kubainisha mambo mawili yanayoathiri utamaduni wa jamii ya Kitanzania. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hilo ulikuwa hafifu kwani watahiniwa 174,069 (12.89%) walipata alama zote 02, watahiniwa 267,696 (19.82%) walipata alama 01 na watahiniwa 908,587 (67.26%) walipata sifuri. Chati Na. 16 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.




**Chati Na. 16**: *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 45*

Watahiniwa 908,587 (67.29%) waliopata sifuri, hawakuelewa matakwa ya swali. Baadhi yao walitoa maelezo yanayohusiana na mila potofu za baadhi ya jamii za Kitanzania. Kwa mfano, *kurithi wajane, mauaji ya vikongwe wenye macho mekundu, vitendo vya watemi wa zamani vya kuzikwa na mtu mzima* na *mauaji ya watoto mapacha*. Majibu hayo yanaakisi matendo mabaya yanayotokea katika jamii. Hivyo, watahiniwa walihusianisha matatizo hayo na neno athiri lililotumika katika kuuliza swali na kuandika majibu hayo yasiyo sahihi.

Vilevile, watahiniwa wachache katika kundi hili, hawakuwa na uelewa wa kutosha juu ya mila na tamaduni za Kitanzania. Waliandika mambo mabaya yanayotokea katika jamii, kama vile; uvivu, matumizi ya bangi, na ulevi wa kupindukia. Kielelezo 5.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyejibu tofauti na matakwa ya swali.


SWALI LA 45


(i) Kukeketa watoto wakike

(ii) Ndoa za utotoni

**Kielelezo 5.1**: *Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 45*

Katika Kielelezo Na. 5.1, mtahiniwa aliandika mambo mabaya yanayofanywa na baadhi ya jamii za Kitanzania, badala ya kubainisha mambo yanayoathiri utamaduni wa jamii ya Kitanzania.

Watahiniwa 174,069 (12.89%) waliandika majibu sahihi. Watahiniwa hao walipata alama za juu (02) katika swali hilo. Ufaulu wa watahiniwa hao ulionesha kuwa walikuwa na maarifa ya kutosha katika kubainisha mambo yanayoathiri utamaduni wa jamii ya Kitanzania. Mambo waliyobainishwa ni pamoja na; *Kukua kwa lugha ya Kiswahili, kukua kwa sayansi na teknolojia, mabadiliko ya mazingira, kukua kwa mwingiliano wa jamii* na *mitandao ya kijamii* (*Utandawazi*). Uelewa mpana katika kujibu swali hili unaonesha kuwa watahiniwa walikuwa na umahiri wa kutosha kuhusu utamaduni na mambo yanayoweza kuuathiri. Sambamba la hilo, watahiniwa 267,696 (19.82%) waliopata alama 01, walidhihirisha uelewa wa wastani juu ya tamaduni za Tanzania kwani walichanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi. Kielelezo 5.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hilo.


SWALI LA 45 i) Utandawazi.
ii) Mwingiliano wa jamii za kigeni.

**Kielelezo 5.2:** *Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 45*

## 3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA KILA UMAHIRI

Umahiri uliotahiniwa katika PSLE 2022 kwa somo la Maarifa ya Jamii na Stadi za Kazi ni; *Kutambua matukio yanayotokea katika mazingira yanayomzunguka, Kutambua misingi ya uzalendo katika jamii, kutumia ramani na elimu ya anga katika maisha ya kila siku, kufuata kanuni za kiuchumi katika shughuli za uzalishaji mali, kusanifu kazi za sanaa, kumudu mapishi mbalimbali, kutumia misingi ya unadhifu na kutumia stadi za ujasiriamali*. uchambuzi unaonesha kuwa, ufaulu wa watahiniwa ulikuwa mzuri katika aina mbili za umahiri ambazo ni;

kumudu mapishi mbalimbali (83.02%) na kusanifu kazi za sanaa (74.59%).

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, ufaulu katika aina nyingine nne za umahiri ulikuwa wa wastani, umahiri huo ni; *Kufuata kanuni za kiuchumi katika shughuli za uzalishaji mali* (54.70%), *Kutumia stadi za ujasiriamali* (49.48%), *Kutambua misingi ya uzalendo katika jamii* (47.49%) na *Kutumia ramani na elimu ya anga katika maisha ya kila siku* (44.07%). Aidha, ufaulu katika aina mbili za umahiri ulikuwa hafifu. Umahiri huo ni *Kutambua matukio yanayotokea katika mazingira yanayomzunguka* (39.42%) na *Kutumia misingi ya unadhifu* (19.38%).

## 4.0 HITIMISHO

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika mtihani wa Maarifa ya Jamii na Stadi za Kazi 2022 umeonesha kuwa, watahiniwa 960,178 (71.08%) walifaulu kwa kupata daraja A – C ambao ni ufaulu mzuri. Ufaulu huo umechangiwa na umahiri waliokuwa nao watahiniwa katika umahiri wa kumudu mapishi mbalimbali, kusanifu kazi za sanaa, kutumia ramani pamoja na uwezo mzuri wa kusoma na kuandika na kuelewa matakwa ya maswali. Watahiniwa 390,596 (28.92%) waliopata daraja D na E walikosa maarifa hayo. Kati ya umahiri uliotahiniwa, ilibainika kuwa ufaulu ulikuwa mzuri katika mahiri mbili, wastani katika mahiri nne na hafifu katika mahiri mbili. Matokeo hayo yanaonesha kuwa, juhudi zinahitajika zaidi ili ufaulu katika mahiri nne zenye ufaulu wa wastani na mbili zenye ufaulu hafifu uongezeke. Ni matumaini ya Baraza la Mitihani kuwa taarifa hii itasaidia mamlaka husika kuchukua hatua stahiki.

## 5.0 MAPENDEKEZO

Ili kuboresha kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika somo la Maarifa ya Jamii na Stadi za Kazi, Baraza la Mitihani la Tanzania linapendekeza mambo yafuatayo;

(a) Ufundishaji na ujifunzanji uzingatie mbinu mbalimbali ikiwa ni pamoja na;

(i) njia ya ziara za kimasomo ili kuwawezesha wanafunzi kujifunza katika mazingira halisi na kuwapa hamasa ya kujifunza zaidi mambo yanayohusiana na zana za mawe za kale, michoro ya mapangoni, biashara ya utumwa, uvamizi wa watu kutoka Asia na Ulaya, vifaa vinavyotumika kupima hali ya hewa na jinsi vinavyofanya kazi. Hii itaongeza ufaulu katika umahiri wa *kutambua matukio yanayotokea katika mazingira yanayomzunguka* na *kutambua misingi ya uzalendo katika jamii.*

(ii) kutumia njia ya majadiliano katika vikundi ili kumjengea mwanafunzi kumbukumbu ya kudumu na ari ya kupenda kujifunza, hasa katika umahiri wa kufuata kanuni za kiuchumi katika shughuli za uzalishaji mali na kutumia stadi za ujasiriamali.

(iii) kutumia michoro, ramani na picha mbalimbali kufafanua dhana mbalimbali wakati wa ufundishaji na ujifunzaji hususani katika umahiri wa kutumia ramani na elimu ya anga katika maisha ya kila siku.

(iv) kufanya matendo mbalimbali ya ujifunzaji kama vile ufinyanzi, ususi, uchongaji, utengenezaji maumbo mbalimbali, ushonaji, upishi wa vyakula mbalimbali, usafi wa mazingira na mavazi ili kuwawezesha wanafunzi kuwa mahiri katika kutumia misingi ya unadhifu, kumudu mapishi mbalimbali na kusanifu kazi za sanaa.

(b) Wanafunzi washauriwe na kusisitizwa kusoma kwa bidii vitabu vya kiada na ziada ili kuongeza maarifa na ujuzi ambao utawawezesha kujibu maswali ya mtihani kwa usahihi.

(c) Mamlaka husika zifanye utafiti wa kubaini changamoto zinazozuia ufanisi katika ufundishaji na ujifunzaji, na kuziondoa ili kuongeza kiwango cha ufaulu.

Kiambatisho

# ULINGANIFU WA UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA KILA UMAHIRI KWA MWAKA 2021 NA 2022

| Na. | Umahiri | Mtihani wa 2021 | | | | Mtihani wa 2022 | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Ufaulu kwa kila Swali | | Wastani wa Ufaulu (%) | Maoni | Ufaulu kwa kila Swali | | Wastani wa Ufaulu (%) | Maoni |
| | | Namba ya Swali | (%) ya Ufaulu | | | Namba ya Swali | (%) ya Ufaulu | | |
| 1. | Kumudu mapishi mbalimbali | 38 | 55.90 | 55.9 | Wastani | 38 | 83.02 | 83.02 | Mzuri |
| 2. | Kusanifu kazi za sanaa | 36 | 57.30 | 57.03 | Wastani | 39 | 74.59 | 74.59 | Mzuri |
| 3. | Kufuata kanuni za kiuchumi katika shughuli za uzalishaji mali | 4 | 50.0 | 33.60 | Hafifu | 1 | 60.20 | 54.70 | Wastani |
| | | 6 | 40.2 | | | 2 | 73.87 | | |
| | | 29 | 35.7 | | | 3 | 19.20 | | |
| | | 30 | 32.7 | | | 4 | 81.62 | | |
| | | 31 | 22 | | | 5 | 52.33 | | |
| | | 32 | 28.9 | | | 6 | 24.59 | | |
| | | 33 | 59.2 | | | 7 | 58.70 | | |
| | | 34 | 19.9 | | | 8 | 57.34 | | |
| | | 35 | 17.4 | | | 41 | 64.47 | | |
| | | 44 | 30.20 | | | | | | |
| 4. | Kutumia stadi za ujasiriamali | 37 | 25.10 | 25.10 | Hafifu | 40 | 49.48 | 49.48 | Wastani |
| 5. | Kutambua misingi ya uzalendo katika jamii | 12 | 87.1 | 41.50 | Wastani | 14 | 27.94 | 47.49 | Wastani |
| | | 13 | 44.9 | | | 15 | 55.09 | | |
| | | 14 | 25.5 | | | 16 | 17 | | |
| | | 15 | 41.0 | | | 17 | 46.58 | | |
| | | 16 | 73.0 | | | 18 | 63.19 | | |
| | | 17 | 76.5 | | | 19 | 62.11 | | |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 18 | 23.4 | | | 20 | 46.49 | | |
| | | 19 | 56.0 | | | 21 | 22.72 | | |
| | | 20 | 15.2 | | | 22 | 68.3 | | |
| | | 21 | 34.6 | | | 23 | 46.48 | | |
| | | 22 | 24.6 | | | 24 | 57.39 | | |
| | | 23 | 25.8 | | | 25 | 71.43 | | |
| | | 42 | 11.5 | | | 45 | 32.71 | | |
| 6. | Kutumia ramani na elimu ya anga katika maisha ya kila siku | 24 | 74.3 | 53.80 | Wastani | 9 | 77.52 | 44.07 | Wastani |
| | | 25 | 47.7 | | | 10 | 59.5 | | |
| | | 26 | 52.0 | | | 11 | 36.34 | | |
| | | 27 | 57.8 | | | 12 | 34.52 | | |
| | | 28 | 40.5 | | | 13 | 19.17 | | |
| | | 45 | 50.2 | | | 42 | 37.39 | | |
| 7. | Kutambua matukio yanayotokea katika mazingira yanayomzunguka | 1 | 10.0 | 39.90 | Hafifu | 26 | 50.67 | 39.42 | Hafifu |
| | | 2 | 65.9 | | | 27 | 17.48 | | |
| | | 3 | 30.4 | | | 28 | 57.49 | | |
| | | 5 | 25.4 | | | 29 | 18.45 | | |
| | | 7 | 46.3 | | | 30 | 28.85 | | |
| | | 8 | 47.6 | | | 31 | 23.86 | | |
| | | 9 | 45.5 | | | 32 | 42.97 | | |
| | | 10 | 50.8 | | | 33 | 43.88 | | |
| | | 11 | 44.2 | | | 34 | 59.09 | | |
| | | 41 | 43.8 | | | 35 | 28.92 | | |
| | | 43 | 15.6 | | | 43 | 53.04 | | |
| | | | | | | 44 | 48.34 | | |
| 8. | Kutumia misingi ya unadhifu | 39 | 63.3 | 39.90 | Hafifu | 36 | 22.00 | 19.38 | Hafifu |